# Nipashe

Jumatatu Julai 1, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581724

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US


**Rais** Nyusi wa Msumbiji atarajiwa kufungua maonyesho ya Sabasaba UKURASA 2



**MFANYABISHARA** maarufu nchini na mdhamini wa zamani wa Klabu ya Yanga, Yusuph Manji amefariki Dunia. UKURASA 5



**Watu** 30 wadaiwa kuuawa maandamno ya Kenya UKURASA 19



**VINICIUS ALALAMIKIA VIWANJA COPA AMERICA** UKURASA 22

MSIGWA KUHAMIA CCM

# Wadau waibuka

• **Lema** atoa ya moyoni asema... *Endelea Ukurasa 2*



Aliyekuwa Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Kanda ya Nyasa na Mbunge wa zamani wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa (kushoto), akiongozwa na Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi, kuingia ukumbini, kabla ya kutangaza rasmi kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakati wa Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), jijini Dar es Salaam jana. **Picha ndogo:** Mchungaji Msigwa, akiwahutubia Wajumbe wa NEC na (kulia) ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Visiwani, Rais wa Zanzibar Dk. Hussein Mwinyi. **PICHA: IKULU**

## Watumishi wawili afya wafa ajali ya bodaboda wakipanda 'mshikaki'

UKURASA 10

## Serikali yatangaza kiama 'vishoka' wanaopangisha nyumba za NHC

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA YANYAKUA KOCHA MOROCCO UK.24 MAONI, UK.6



Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje (CHADEMA), John Mrema



Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini ,Godbless Lema **PICHA ZOTE: MTANDAO**

# Msigwa kuhamia CCM wadau wa siasa waibuka

**Na Mwandishi Wetu**

BAADHI ya wanasiasa na wachambuzi wa siasa wamesema uamuzi wa aliyekuwa Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Nyasa, kuhamia Chama Cha Mapinduzi (CCM) unatoa tafsiri nyingi ikiwamo nia ya dhati ya kuwa mpinzani nchini.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, walisema kiongozi huyo ametumia haki yake kuhama kama ilivyo kwa wachezaji wa mpira, huku wengine wakiona ni anguko la kisiasa hasa kwa wakati alioondoka kwenye chama chake.

Mwenyekiti wa CHADEMA Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema alisema: "Nimeumia sana, alikuwa 'colleague' nimekaa naye bungeni, nimekwenda jimboni tumeshirikiana, tamaa yangu kubwa kwamba ningefanya naye kazi CHADEMA kuliko huko alikokwenda, sikutarajia japo nilifahamu alikuwa na hasira kali, nahisi huenda kuna kitu sikufanya kwa rafiki yangu.

"Alikuwa ni 'partner' kwenye 'struggle' sioni sawa kwa Msigwa kwenda kufanya kazi na CCM, katika siku za mwisho za kuiondoa CCM madarakani," alisema.

"Huenda alikuwa na hasira kali sana mabayo huenda sikuielewa, ningejua ningetumia muda wangu kama rafiki kumshauri huenda asingeenda," alisema.

Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itifaki na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, alisema chama kilikuwa na taarifa za kiintelejensia kwamba hana muda mrefu ataondoka, na kwamba vurugu zote alizokuwa anafanya kule Kanda ya Nyasa ili kuwa ni maandalizi kuelekea CCM.

"Chama tulishaona, tunatarajia atazungumza mambo mengi ya kweli na yasiyo ya kweli atayaacha, tunawataka wanachama wetu kule Nyasa kuendelea na maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa. Yeye sio wa kwanza kuhama walikuwapo wengi maarufu kuliko yeye waliondoka na chama hakikuwahi kuyumba na tunaendelea kujenga chama."

Mwenyekiti wa BAWACHA Mkoa wa Morogoro, Devotha Minja alisema: "Ninachokiona kuwa mpinzani kwa miaka mingi halafu unatimka kisa umekosa nafasi ya kanda sio sawa, maana yake tulikuwa na mtu ambaye sio mpambanaji, hakuwa na nia ya dhati, kwasababu alichokuwa anakipinga ni serikali leo ameamua kuungana nayo, maana yake hakuwa mpigania haki kwa Watanzania.

Aliyekuwa Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Boniface Jacob alisema: "Sidhani kama ni uamuzi sahihi kwa namna yoyote, kwanza kahama kipindi kibaya kwasababu kashindwa uchaguzi, kila mtu anajua kwamba kashindwa uchaguzi.

"Mtu akihama kwa sasa sio msimu mzuri ni kama amesubiri jua au mvua inyeshe ndio atoke, kipindi cha nyuma walikuwa wanapewa ofa mbalimbali. Mwenendo wake ulionyesha alishakata tamaa,"alisema.

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. George Kahangwa, alisema mwanasiasa kuhama kutoka chama kimoja kwenda kingine ni jambo la kawaida, na kwamba ni haki yake mtu yeyote kwenye chama.

Alisema anachokiona ndani ya chama hicho ni matokeo ya kutoelewana kwao katika chaguzi za ndani ya chama, na wasingeweza kuendelea kukaa pamoja labda kama pangefanyika jitihada za kumaliza mgogoro.

"Moja ya matatizo tuliyonayo ndani ya vyama hakuna mfumo wa kumaliza tofauti na watu waende vizuri, kwenye chama chochote unapogombea nafasi atatokea mmoja ashinde na mwingine anakosa, kama chama kingekuwa na utaratibu wa kuwaweka sawa mambo maana yake wangeyazungumza ndani kwa ndani," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kahangwa, Msigwa hawi mwanasiasa wa kwanza kwa kuwa wapo wengi walitoka wakaenda CCM au CHADEMA, na kwamba siku zote wanasiasa ni watu wa kuvizia fursa, hivyo ameona katika uchaguzi mkuu kuna mambo yanaweza kwenda vizuri kwake.

"Siasa ni kama mpira leo ni mchezaji wa timu fulani kesho ni nyingine. Lakini wanasiasa wetu pamoja na haki yao ya kuhama wakumbuke kuwa wakweli, ukisikiliza 'speech' (hotuba) zake ikiwamo neno maarufu la 'You guys are tired' ambalo alilitumia sana akiwa bungeni, usingefiri kwa kauli hizi angekuwa ni mtu angefika mahali akaondoka, ingawa ni haki yake," alifafanua.

Alisema wanasiasa wanapaswa kuwa na busara ya kuwa mtu kutamka masuala yanayohusu maslahi ya watu bila kuponda wengine ambao kesho atajiunga nao na ni hekima inayopaswa iwaongoze wanasiasa wetu, kwa kuwa ukiitukana CCM halafu kesho ukahamia huko unakuwa umepoteza kuaminika.

Mchambuzi wa siasa na Mwanadipolomasia, Hamduni Maliseli alisema: "Inaonyesha dhahiri watu tulionao (wanasiasa) ni watu wa ina gani dhidi ya upinzani, wamekaa kwenye upinzani kwa ncha za vidole na sio mguu kamili, kwasababu hakupata fursa ya kuwa katika uongozi basi kaenda CCM."

"Hii inaonyesha upinzani wa baadhi ya watu hauna uhalisia ni matokeo ya kusaka tonge akikosa kulia apate kushoto. Msigwa amekuwa kiongozi aliyeaminika sana kwenye jamii, kitendo cha kuhama kwasabau ya kukosa uongozi, inaoyesha tu safari, bado kuna mzaha na hakuna watu wanaoamini katika itikadi na falsafa ya chama fulani kwa dhati ya moyo ndio mana wanachomoka hovyo," alibainisha.

Kwa mujibu wa mchambuzi huyo, Msigwa kwenda ni haki yake, lakini tatizo ni mtu wa aina gani, ana nafasi gani, alizungumza mangapi kuhusu uimara na uthabiti wa upinzani, nguvu yake na kwamba asipoangalia inaweza kuwa ndio mwisho wake.

"Taswira sio upinzani bali hata nafsi inaweza kumsuta hata yeye mwenyewe," alisema.

Mwandishi wa habari nguli, Absalom Kibanda alisema: "Nimejifunza kwamba usiwapime wanasiasa kwa maneno yao bali kwa kauli zao, kauli zake zilionyesha ndiye anakerwa sana na watu wanaohama kwenda CCM, alimkosoa sana Mwenyekiti wake Freeman Mbowe alivyokwenda kuonana na Rais Samia Suluhu Hassan, na kila mahali alisema angehama enzi za Rais Dk. John Magufuli, alionyesha ni mwanaCHADEMA kindakindaki."

"Ila inanikumbusha kauli ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere kwamba CCM sio baba yangu wala mama yangu," alisema.

Kibanda alisema Msigwa alikuwa Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa aligombea na kushindwa maana yake angeshinda angeendelea kubaki na alikata rufani kudai haki yake leo anahamia CCM inaibua maswali mengi kuhusu siasa na wanasiasa wa vyama vingi.

Msigwa ambaye ni Mbunge mstaafu wa Jimbo la Iringa Mjini, alitangaza uamuzi wa kukihama CHADEMA, alipokewa jana wakati wa Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (NEC), kilichoketi chini ya Mwenyekiti wake, Samia Suluhu Hassan.

## Rais wa Msumbiji atarajiwa kufungua maonyesho Sabasaba

**Na Jenifer Gilla**

RAIS wa Msumbiji, Filipe Nyusi, anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika ufunguzi wa Maonyesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), maarufu Sabasaba Julai 3, mwaka huu.

Pia, anatarajiwa kufanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais Samia Suluhu Hassan, yanayolenga kukuza biashara, uwekezaji, ulinzi na usalama.

Akizungumzia ugeni huo jana, Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, alisema Rais Filipe anatarajiwa kuwasili nchini leo kwa ziara ya siku nne kwa mwaliko wa Rais Samia.

Alisema atakapowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA), Rais Nyusi atapokewa na viongozi waandamizi wa serikali na Julai 2, atapokewa rasmi Ikulu ya jijini Dar es Salaam.

"Wakiwa Ikulu marais hao watafanya mazungumzo ya faragha na rasmi yatakayojikita katika kukuza biashara, uwekezaji, ulinzi na usalama," alisema.

Kwa mujibu wa Waziri January, mazungumzo hayo yatafuatiwa na utiaji saini wa mikataba ya ushirikiano katika sekta za ulinzi, usalama, elimu, nishati, habari na uchumi na kuzungumza na waandishi wa habari.

Alisema pia ziara hiyo inalenga kujadili namna ya kukabiliana na changamoto za kiusalama katika mipaka ya nchi hizo kwa muda mrefu.

"Julai 3, Rais Filipe anatarajiwa kuwa mgeni rasmi katika maonyesho ya Sabasaba katika Viwanja vya Mwalimu Nyerere, Dar es Salaam. Kisha atakwenda Zanzibar kwa ziara binafsi na kurejea Msumbiji Julai 4," alisema.

Waziri huyo alisema ziara hiyo itakuwa ni ya mwisho kwa Rais huyo kama kiongozi wa nchi na atatumia nafasi hiyo kumuaga Rais Samia na Watanzania kwa kuwa atamaliza muhula wa pili wa urais Octoba, mwaka huu, baada ya kuiongoza kwa miaka 10 tangu 2015.

Alisema uhusiano uliendelea kuimarika na mwaka 1977 nchi hizo zilisaini makubaliano ya kuanzisha Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) ambayo imeshafanya mikutano 15.

"Kupitia mikutano hii, nchi hizi zimekubaliana kushirikiana katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ulinzi na usalama, uhamiaji, biashara, uwekezaji, utalii, kilimo na uchukuzi," alisema January.

Aidha, Tanzania imekuwa mstari wa mbele kuisaidia nchi hiyo kukabiliana na changamoto za kiusalama. Ikiwa ni moja kati ya nchi 11 za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) zilizochangia vikosi vya kulinda amani kutokana na mashambulizi ya vikundi vya kigaidi Kaskazini mwa nchi hiyo, hasa katika majimbo ya Cabo Delgado, Niassa na Nampula.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yawatangazia 'kiama' wanaopangisha nyumba za NHC

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imeliagiza Shirika la Nyumba (NHC), kufanya msako wa kuwaondoa watu wanaofanya udalali wa nyumba zake kwa kuzichukua na kuwapangisha watu wengine kwa gharama kubwa.

Agizo hilo lilitolewa jana na Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geofrey Pinda, baada ya Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kutembelea miradi ya shirika hilo jijini Dar es Salaam ya Samia Housing Scheme Kawe, Morocco Square na mradi wa 711.

"Nyumba nyingi za NHC zimegeuzwa kuwa mradi wa watu waliokuwa wapangaji wa shirika kwa hiyo nimeiagiza NHC ifanye ukaguzi wa kina kuwabaini watu walioanza kukaa kwenye nyumba hizo na kama ndio wanaoendelea kukaa humo au la," alisema.

"Na hao ambao wamepewa na waliokuwa wapangaji NHC wajulikane ili waweze kupewa upangaji rasmi badala ya kuwa wanawalipa fedha nyingi watu ambao hawahusiki na nyumba hizi za serikali na nimeambiwa kwamba wanachukua fedha nyingi sana hawa kwa kuwapangisha watu," alisema.

Pinda alisema baadhi ya watu wamechukua nyumba zaidi ya 10 na kuwapangisha wananchi kwa gharama kubwa hali ambayo alisema serikali haiwezi kuifumbia macho.

Alisema wapangaji lazima walipe kwa wakati kwa kuwa wanapochelewa kulipa pango ndani ya makubaliano ya mkataba na mpangishaji wanasababisha usumbufu.

Kuhusu maendeleo ya miradi hiyo, Pinda alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia miradi hiyo kuendelea baada ya kusimama muda mrefu kutokana na sababu mbalimbali zilizoelezwa.

Alisema kamati imeridhika kuona majengo mengi yamekamilika na wapangaji wameanza kuingia na wengine kununua nyumba kwenye majengo hayo.

Mkurugenzi wa NHC, Hamad Abdallah alisema mradi wa Samia Housing Scheme wa Kawe wenye nyumba 5,000 unaendelea lakini zote zimeshanunuliwa na wananchi.

Alisema kwa sasa NHC inajipanga kuanza ujenzi wa awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba 500 eneo la Kawe na kuongeza kuwa wabunge pia wanajionea maendeleo ya miradi wa nyumba za 711 ambazo ujenzi wake ulisimama kwa miaka mingi.

"Wakati mradi huu unasimama ujenzi ulikuwa ghorofa ya saba, lakini kwa sasa tuko ghorofa ya 12 na ujenzi unaenda kwa kasi na mauzo ya nyumba yameshaanza na ndani ya miezi mitatu tumeshapata shilingi bilioni tatu," alisema.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Timotheo Mzava, alisema wameridhishwa na maendeleo ya miradi hiyo yote mitatu ambayo kukamilika kwake kutasaidia wananchi wengi kupata makazi nafuu.

"Miradi hii isingefikia hatua hii tunayoona leo kama sio nia ya dhati ya Rais Samia Suluhu Hassan kuwezesha NHC kupata fedha za kuendelea na miradi na sisi tumewaambia kwamba hawana kisingizio tena kwani fedha zimetolewa wafanye kazi," alisema.

"Hakuna sababu yoyote ya kukwamisha miradi hii kwasababu fedha wameshapewa kwa hiyo sisi tumewasisitiza wasimamie ujenzi huu na hatutaki kuona tena miradi hii inasimama," alisema Mzava

# Kicheko wakulima wakiuza ufuta zaidi tani 4,000

**Na Said Hamdani,** LINDI

JUMLA ya tani 4,405 na kilo 472,183 za ufuta zimeuzwa katika Halmashauri za Kilwa, Mtama na Manispaa ya Lindi katika mnada wa Chama Kikuu cha Ushirika Lindi Mwambao mkoani hapa kupitia mfumo wa Soko la Biashara Tanzania (TMX).

Mnada huo wa pili uliofanyika Kijiji cha Njinjo, Wilaya ya Kilwa umehusisha ufuta wa kwenye maghala ya Nangurukuru Halmashauri ya Kilwa, Bucco, Hazina Manispaa ya Lindi na Ilulu, Halmashauri ya Mtama.

Akitangaza viwango vya bei zilizofikiwa na kampuni zilizojitokeza kununua ufuta huo, Ofisa TEHAMA Goodluck Luhanjo, alisema maghala ya Hazina na Ilulu yaliyopo Halmashauri ya Mtama, yameongoza kwa kuwa na kiwango cha bei za juu.

Akizungumza na wakulima waliojitokeza kwenye mnada huo, alisema ghala la Hazina lilikuwa na tani 510 na kilo 531,021 bei ya juu Sh. 3,482 ya chini Sh.3,450 na Ilulu yenye tani 549 na kilo 854,000 Sh. 3,490 bei ya juu na ya chini Sh.3,400/-.

Ghala la Bucco lililopo Manispaa ya Lindi, tani 1,510 sawa na kilo 1,510,338, bei ya juu Sh. 3,470 na ya chini ni Sh. 3,400, wakati ghala la Nangurukuru lenye tani 1,826 na kilo 1,826,824, bei ya juu imefikia Sh. 3,440 na ya chini ni Sh. 3,340 kwa kila kilo moja.

Mnada umeendeshwa kwa mfumo wa Soko la Biashara Tanzania (TMX), tofauti na ilivyozoeleka kwa wanunuzi kuandika barua wakitaja kiwango wanachokihitaji na bei na kutumbukiza kwenye sanduku, ambalo hufunguliwa na kusomwa na kutajwa bei mbele ya wakulima na wanunuzi wakiwapo siku ya mnada.

Katika mnada huo, kampuni zinazofika bei za juu hupewa fursa kununua mzigo, lakini kwa sasa hufanyika kidijitali kwa njia ya mfumo unaoendeshwa na TMX na kiwango cha tani za ufuta hurushwa mtandaoni, wanunuzi wakishindana kwa kuongeza kiwango cha fedha wanazozinadi na wakulima wakishuhudia kupitia mtandaoni.

Wakizungumza na mwandishi wa habari hizi, wakulima Juma Hemedi, Juma Yusufu, Mwanahawa Ismaili, Somowe Abdallah na Hamida Saidi, walisema hawaridhishwi na bei zilizofikiwa na kampuni hizo, lakini wamekubali kuuza kwa shingo upande.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian


KILIMANJARO
DRINKING WATER
A PRODUCT OF
The Coca-Cola Company
Mshindi wa
SUPERBRANDS
AFRIKA MASHARIKI
2022-2024
VOTED
Superbrands
EAST AFRICA'S CHOICE
2022-2024
Asanteni wateja wetu
Hii ni yetu sote
kilimanjaro_drinking_water
kilimanjarodrinkingwater
kdw@bbl.co.tz
+255 762628166 | +255 659785276 | +255 272754422



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (kulia), akikabidhi zawadi kwa mshindi wa kwanza wa mashindano ya kusoma Kurani, Ismail Khalid wakati wa hafla ya kumbukumbu ya kuanzishwa kwa Taasisi ya Maawal Islamiy na Mwanzilishi wake, Sheikh Shabaani Mohamed Hariri, jijini Tanga mwishoni mwa wiki. **PICHA: WMNN**

# Manji afariki Dunia

**Na Adam Fungamwango**

MFANYABIASHARA maarufu nchini, Mwenyekiti na mdhamini wa zamani wa Klabu ya Yanga, Yusuph Manji amefariki Dunia.

Taarifa za kifo hicho zimethibitishwa na mtoto wake, Mehboub Manji, ambaye amesema Mkurugenzi huyo wa Kampuni ya Quality Group Limited, alifariki dunia Jumamosi Juni 29, saa 6:00 usiku katika Jimbo la Florida nchini Marekani alipokuwa anapatiwa matibabu.

Manji pia aliwahi kuwa, Diwani wa Kata ya Mbagala Kuu kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mfanyabiashara huyo atakumbukwa zaidi na wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwani aliirudisha kwenye hadhi yake baada ya kukumbwa na migogoro ya mara kwa mara.

Aliingia Yanga mwaka 2006 kama mdhamini kupitia kampuni yake moja ya bahati nasibu, baadaye akawa mfadhili Mkuu wa klabu kabla ya kuwa Mwenyekiti.

Katika kipindi chake cha kuwa mfadhili na Mwenyekiti wa Yanga, atakumbukwa kwa kuirejeshea hadhi na heshima klabu hiyo.

Alipoingia aliikuta klabu ilipodhoofu kiuchumi na haiwezi kushindana na mahasimu wao, Simba katika kuwania wachezaji bora ambao ndiyo mtaji wa kushinda mataji.

Moja ya wachezaji ambao waliwasajili kwa kishindo ni kutoka kwa mahasimu wao wa jadi Simba ni Emmanuel Okwi, Kelvin Yondani, Juma Kaseja na ikawapora mchezaji Mbuyu Twite ambaye alikuwa ameshatangazwa na Wekundu wa Msimbazi kutokea, APR ya Rwanda, lakini akaibukia Jangwani.

Baada ya mafanikio makubwa, alijiondoa rasmi kwenye klabu hiyo, 2017, na kuifanya klabu hiyo kuyumba kiuchumi na katika kusaka fedha ilianza kuanzisha Harambee, iliyopachikwa jina la 'bakuli' hadi pale Kampuni nyingine ya GSM ilipoingia.

# JKCI mbioni kufungua kitengo cha moyo Arusha

**Na Beatrice Shayo,**
ARUSHA

MKURUGENZI Mtendaji wa Taasisi ya Jakaya Kikwete (JKCI), Dk. Peter Kisenge, amesema wapo katika mchakato wa kuanzisha kitengo cha moyo Mkoa wa Arusha ili kutoa matibabu kwa ukaribu zaidi.

Kisenge aliyasema hayo jana mkoani hapa wakati akizungumza na wananchi waliojitokeza kwenye kambi ya matibabu bure inayotarajia kumalizika leo, huku akieleza kuwa kituo hicho kitakuwa na mitambo mikubwa ya upasuaji.

"Tutakuwa na mitambo mikubwa ya upasuaji wa moyo na kuweka klabu, tayari fedha tumeanza kuzitafuta tutakuwa na kitengo cha moyo na kuwatibia mikoa yote ya pembeni," alisema Dk. Kisenge.

Alisema kwa matukio aliyoyaona katika kambi hiyo, magonjwa ya moyo kwa Mkoa wa Arusha yana takwimu kubwa na kuanzia Septemba watakuwa na kliniki itakayoshirikiana na wataalamu wa Jiji la Arusha kutoa huduma.

Aidha, aliwaomba wananchi kufanya mazoezi mara tatu kwa wiki kwa kuwa yatasaidia kuwalinda wasipate maradhi ya ugonjwa wa moyo.

Alisema kwa upande wa moyo wamewaona zaidi ya watu 1,500 kati ya hao asilimia 40 wamekutwa na matatizo mbalimbali na wengine wana shida ya umeme wa moyo.

"Kuna mgonjwa ambaye nilimkuta ana mapigo ya moyo chini ya 39 alikuwa hajijui. Mwanadamu ili aweze kuishi anatakiwa mapigo yake yaanzie 60 na kuendelea yeye alikuwa na 39 tumemkimbiza Dar es Salaam kwa matibabu zaidi," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Kisenge, kama asingefika katika kambi hiyo huenda angepoteza maisha ghafla na watu wa aina hiyo wengi hupoteza maisha wakiwa wamelala.

Aidha, alisema wagonjwa 183 waliokuwa na matatizo ya moyo wamepelekwa JKCI na wote wanalipiwa na Rais Samia Suluhu Hassan na hakuna atakayekosa huduma.

Aidha, wamewaona watoto 150 waliokuwa na matatizo mbalimbali kati yao 53 wanatakiwa kufanyiwa upasuaji mkubwa wa moyo.

Alisema watoto hao watapelekwa Mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya upasuaji na kila mtoto mmoja kufanyiwa upasuaji ni Sh. milioni 12, matibabu hayo yatagharamiwa na Rais Samia.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda, alisema amepata faraja kubwa kutokana na siku saba za kutoa matibabu na kuwafikia zaidi ya watu 30,000.

Makonda alisema wamekubaliana na madaktari wa mkoa na timu inayotoa huduma kuongeza siku moja kwa ajili ya wale ambao wana namba wapatiwe huduma.

"Itakuwa haina maana mwananchi amekuja tangu Alhamisi na wengine wamelala kwenye huu uwanja warudishwe nyumbani bila kutibiwa hili sio jambo la haraka yaani unaingia na kutibiwa kuna baadhi ya sampuli zimepelekwa mkoani wa Dar es Salaam ili wapatiwe majibu," alisema.

Aidha, Makonda aliahidi kutafuta wadau wamsaidie viti mwendo kwa ajili ya watu 1,000 na watafikiwa kwenye kila wilaya.


**BISMILLAH RAHMAN RAHIM**



Familia ya marehemu **DK. Omar Ali Juma** inapenda kuwakaribisha kwenye Hitima ya kumuombea Marehemu **DK. Omar Ali Juma** itakayofanyika siku ya Alhamisi tarehe **4 Julai, 2024** saa kumi jioni katika Msikiti wa **Ngazija.**

Kufika kwenu ndio mafanikio yetu.

Ndugu, Marafiki na Jamaa wote mnakaribihswa.

**Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. AMIN**

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kanuni hii ipitishwe Ligi Kuu kukomesha imani za kishirikina

**TAYARI** Bodi ya Ligi Kuu imeendelea kupokea maoni kwa ajili ya maboresho la Kanuni za Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2024/25.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa Bodi ya Ligi, Karim Boimanda, hivi karibuni alisema wameendelea kupokea maoni kwa njia mbalimbali za mawasiliano, huku akiahidi kuwatembelea pia wadau wa soka, vikiwamo vyombo vya habari kwa ajili ya kupata mawazo mengi zaidi yatakayofanya kuwe na kanuni bora msimu ujao.

Alikiri kuwa eneo la imani za kishirikina ndilo lililoonekana kuvutia wadau wengi kutoa maoni yao kuliko kanuni zingine.

Pamoja na mambo mengine, sisi tunaona imefika wakati sasa jambo hili lifanyiwe kazi kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu, ili hata kama halikuisha, tuone likipungua kwa kiasi kubwa kwani linachafua sana ligi yetu ambayo kwa sasa ni ya sita kwa ubora barani Afrika.

Hii ni kutokana na kuona ni kosa ambalo limekuwa likijirudia kama ambavyo wenyewe Bodi ya Ligi wanavyobainisha.

Kwa ujumla haturidhishwi na adhabu za faini zinazotolewa, ambapo klabu hazishtuki na hazioni shida kuilipa, hivyo kurudia mechi baada ya mechi, huku taarifa zikieleza hata hizo faini zenyewe hukatwa kwenye viingilio vya mechi.

Tunadhani umefika wakati sasa kupitishwa kanuni kwa klabu itakayobainika na kuthibitishwa imefanya vitendo hivyo ikatwe angalau pointi moja kwani suala la faini sasa linaonekana kuwa la kawaida kwao.

Pointi moja tu, inatosha kuitoa timu kwenye reli na isirudie tena mchezo huo, na kama hiyo haitoshi basi ikiwezekana iwe pointi na faini pia.

Kuzikata pointi ndiyo adhabu pekee inayoweza kuzitisha klabu kuacha mtindo huo kwani viongozi watawajibika kwa wanachama na mashabiki wao.

Timu inapokatwa pointi halafu ikaachwa nyuma na wenzake, au kuukosa ubingwa kwa sababu ya pointi moja au mbili zilizokatwa kwa sababu ya vitendo vya kishirikina, viongozi watakuwa na cha kujibu kwa wanachama na mashabiki wao.

Tunaamini kwa sasa viongozi wa klabu hizi hawaogopi adhabu hii kwa sababu nyingi sana. Chache ni kwamba haziwaumizi, yaani kuwanyang'anya ushindi wanaoupata, lakini pia hata pesa zenyewe hawatoi mfukoni, bali ni zile zinazokatwa moja kwa moja timu zao zinapocheza.

Tena klabu kubwa kama za Simba na Yanga huwa hazisikii maumivu kabisa kwani zinavuna pesa nyingi za kiingilio cha mashabiki, kwa hiyo hata pesa inayokatwa kwao hazioni tatizo.

Tunatambua maana ya adhabu ni kumfanya mtu ajutie kile ambacho alikitenda na asikirudie tena, hivyo ukiona mtu anapewa adhabu halafu anarudia tena na tena, ujue hiyo kwake siyo adhabu, unapaswa kubadilisha.

Kwa sababu lengo la kufanya vitendo vya kirishikina, kuingia kwenye mlango usioruhusiwa, kuruka ukuta na kufanya chochote kinachoonyesha kuwa si cha kawaida, ni kusaka ushindi, yaani pointi tatu, hivyo utakapozipata na kisha ukazinyang'anywa ulichokifanya hutakirudia tena.

Kama Bodi ya Ligi ikipitisha kanuni hiyo na kuisimamia ipasavyo, tunaamini wahusika wataacha vitendo hivyo.

Ila katika hilo tunapendekeza pia timu isikatwe kama vitendo hivyo vinafanywa na mashabiki badala yake wao nao wapate adhabu yao peke yao, kwani kwa kufanya hivyo kunaweza kujitokeza mashabiki wa upande wa pili wanaoweza kuvaa jezi za mpinzani wao kwa lengo la kwenda kuiharibia kwa kujifanya wanafanya vitendo hivyo vinavyoashiria ushirikina.

Hii ni kwa sababu kwenye soka la Tanzania kuna kitu kinaitwa kuhujumiana, inawezekana watakaofanya hivyo ikawa si mashabiki halisi wa timu ile.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Klabu zitumie 'pre season' kujenga vikosi kuwa imara

Na Adam Fungamwango

**YANGA** ilianza Ligi Kuu msimu uliopita kwa kuitwanga KMC mabao 5-0 katika mechi ya kwanza ya ufunguzi.

Simba nayo iliiadhibu Mtibwa Sugar mabao 4-2, ikiwa pia ni mechi ya ufunguzi, raundi ya pili Yanga ikarudia kile ilichokifanya raundi ya kwanza, ikiifanyia mauaji JKT Tanzania kwa idadi kama ile ile ya mabao 5-0 iliyoifunga KMC.

Labda hapa tujiulize ni kwa nini timu hizo zilichapika mabao mengi mwanzoni tu mwa msimu.

Ukweli ilionekana hazikufanya maandalizi mazuri ya msimu, na kwa bahati mbaya sana zinakutana na timu kubwa na ngumu.

Siyo hizo tu, hata kama zingekuwa timu zingine ambazo zingekuwa hazijafanya 'pre season' yao vizuri zingepigwa nyingi.

Vipigo vile vinazikumbusha klabu zinazojiandaa na msimu mpya wa mashindano kwenda kujiandaa kisawasawa na wiki hizi za kambi ya mwanzo, inayoitwa kwa lunga la kigeni 'pre season.'

Hiki ni kipindi cha kutengeneza timu bora ya msimu mzima, na iwapo kitachezewa basi wachezaji hawatofanya vema msimu mzima.

Hiki ni kipindi cha wachezaji kutengeneza pumzi, na stamina ambayo humfanya kuweza kuhimili mikikimikiki ya msimu mzima wa ligi na mashindano mengine.

Ni kipindi ambacho wachezaji hufanya mazoezi magumu kuliko yote watakayoyafanya baada ya hapo, kwani watakachotakiwa ni kuilinda pumzi na stamina iendelee kuwapo na si kuitafuta tena.

Mchezaji anapoyakosa au kutoyafanya sawasawa, hata awe na kipaji kizuri vipi hawezi kuwa bora au kwenye kiwango chake kilichozoeleka kwa msimu mzima.

Moja ya vitu vilivyoisaidia zaidi Yanga misimu hii mitatu kutwaa ubingwa ni wachezaji wake kuwa na utimamu mzuri wa mwili.

> **Huwezi kuwa na wachezaji kambini kipindi cha 'pre season' halafu ndiyo unatafuta kocha, au unaye lakini bado hajawasili kwa sababu hajalipwa chake, au ndiyo unaendelea kusajili.**

Ndiyo maana hata wale ambao hawakuwa sehemu ya kikosi cha kwanza, bado walikuwa na msaada mkubwa wanapoingia kwani hata kama hana kiwango kikubwa sana, lakini fiziki ilikuwa inawasaidia kutimiza malengo.

Simba ilikuwa ni timu ambayo haikuwa na utimamu mkubwa sana wa mwili kwa wachezaji wake, na ulikuwa unashuka kile mechi zinavyoendelea.

Nazishauri klabu ambazo mwezi huu wa saba zinaanza maandalizi kuwa siyo kipindi cha mbwembwe na 'pikniki', bali ni cha kujiweka fiti kwa msimu unaokuja.

Kwa viongozi hiki ni kipindi ambacho wanatakiwa kuwa wamekamilisha vitu vyote kuanzia usajili, makocha mpaka vifaa vya mazoezi, ili kuepusha kile kilichoonekana msimu uliopita baadhi ya timu zikiwa mpaka na wachezaji watano tu kambini, wengine hawajaja kwa kutopewa pesa zao za usajili, au kuendelea kusajili.

Hiki siyo kipindi cha kufanya usajili na mchezaji anakuja siku chache kabla ya maandalizi kukamilika.

Siyo kipindi ambacho klabu inakuwa na wachezaji halafu haina kocha ambaye anakuja wiki moja kabla ya ligi kuanza.

Klabu yoyote itakayofanya hivyo, haitofanya vema kwenye ligi kwani kinakuwa ni kipindi cha kucheza mechi, kutengeneza mfumo wa kukabiliana na timu husika na kusafiri tu, si cha kutengeza fiziki.

Mara nyingi viongozi wa klabu wanakosea kufanya hivi, badala yake zigo wanawaangushia makocha.

Huwezi kuwa na wachezaji kambini kipindi cha 'pre season' halafu ndiyo unatafuta kocha, au unaye lakini bado hajawasili kwa sababu hajalipwa chake, au ndiyo unaendelea kusajili.

Nadhani viongozi wa klabu wanatakiwa wanielewa, ili ligi ikianza msiseme kuwa sijawaambia.

HABARI KITAIFA

# Biteko ataka mkakati kuinua makandarasi

Na Joseph Mwendapole

NAIBU Waziri Mkuu, Dk. Doto Biteko, ameielekeza Wizara ya Ujenzi kuweka mkakati wa kuwainua makandarasi nchini, pamoja na mpango mzuri wa taasisi za fedha kuwakopesha ili wakuze mitaji yao.

Aidha, amesema makandarasi hao wakikuza mitaji yao watajenga miradi mikubwa kama wenzao wa nje.

Aliiagiza wizara hiyo kutekeleza mkakati huo ipasavyo kuanzia ngazi ya Wizara ya Ujenzi pamoja na Wizara ya Fedha.

Alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam wakati wa kufunga kongamano la makandarasi na watoa huduma, lililoandaliwa na Chama cha Umoja wa Makandarasi na Watoa Huduma Shirikishi Tanzania (TUCASA).

Alisema katika mpango mkakati wa kukuza makandarasi wa ndani kuwekwe kipengele cha kuhakikisha miradi yote inayotekelezwa kwa fedha za mikopo kutoka kwa wadau wa maendeleo kunatengwa asilimia isiyopungua 20 kwa ajili ya makandarasi wa ndani.

Aidha, alisema dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuwajengea uwezo makandarasi wazawa na alitoa maelekezo kwa viongozi wote wa serikali pamoja na watumishi wa ngazi zote kuhahakikisha wanatekeleza agizo hilo.

Kadhalika, Dk. Biteko aliwataka makandarasi nchini kutekeleza miradi ya ujenzi kwa ubora na uzalendo mkubwa, ili wainue uchumi wa nchi na kuhakikisha wanatekeleza miradi mikubwa.

Pia, aliwataka waheshimu matumizi ya fedha za miradi, kwa kufanyia shughuli za ujenzi na faida watakayoipata waiwekeze kama mkakati wa kukuza mitaji ya kampuni zao.

Alisema ofisi ya waziri mkuu itaelekeza sekta zingine zikiwemo za nishati, maji na uchukuzi, kuhakikisha zina wapa upendeleo makandarasi wazawa pamoja na kuwawekea malengo.

Alisema kwenye mikutano yao ya kila mwaka wapime utekelezaji wa malengo hayo na kama kuna changamoto basi waweke mikakati ya kuzitatua ili waweze kukua kwa haraka.

Aidha, aliitaka wizara ya ujenzi kuiga mfano wa kuwaendeleza vijana wa wizara ya kilimo uitwao 'Build Better Tomorrow' (BBT), kwa kuwasaidia vijana kuanzisha kampuni na kuwapatia kazi ndogo ndogo ili kuwajengea uzoefu.

Dk. Biteko pia alisisitiza kuwa serikali imeendelea kuwachukulia hatua watumishi wote wa umma wanaobainika kujihusisha na vitendo vya rushwa.

"Napenda niwahakikishie kuwa serikali kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (TAKUKURU), itaendelea kuchukua hatua za kisheria kwa watumishi wanaojihusisha na rushwa. Ombi langu kwenu mnapokutana na tatizo la rushwa msisite kutoa taarifa TAKUKURU," alisema Dk. Biteko.

Waziri wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, alisema Rais Samia anatambua mchango wa makandarasi wazawa nchini na anataka kuona wanakuwa mstari wa mbele katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya ujenzi hapa nchini.

Mwenyekiti wa TUCASA, Samwel Marwa, aliiomba serikali iwe mlezi kwa TUCASA, ili kuwajengea uwezo wa kufanya miradi mikubwa ya ujenzi kwa kuisimamia wenyewe.

Pia aliiomba serikali kuendelea kupambana na rushwa ili makandarasi wazawa wapate zabuni kubwa za ujenzi na hatimaye kukuza kampuni zao.



Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Udhibiti wa taka ngumu wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro (kushoto), akiwasaidia wafanyakazi wa jiji hilo, kupakia taka kwenye gari kandokando ya barabara ya soko la Sabasaba jijini humo, jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# 'Makundi maalum changamkieni zabuni serikalini'

Na Restuta James

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, amewataka wanawake, vijana na wenye ulemavu, kuchangamkia zabuni za serikali kwa kuwa asilimia 30 ya bajeti yote ya ununuzi wa umma, imetengwa kwa ajili ya makundi hayo.

Beng'i aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, alipokuwa akizindua Programu ya BID for success (B4S), inayoratibiwa na Chemba ya Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), kwa lengo la kuwajengea wanawake na vijana uwezo wa kushiriki zabuni za serikali, kwenye sekta mbalimbali.

Alisema ununuzi wa umma unatumia asilimia 80 ya bajeti ya matumizi ya serikali, akieleza kuwa asilimia 30 inayotajwa kwenye kanuni za Sheria ya ununuzi ya umma inafikia Shilingi trilioni mbili kwa mwaka.

"Kama tutazipata zikaingia kwenye biashara zetu zitachochea sana ukuaji wa uchumi wenye matokeo makubwa. Nataka niwape hiyo changamato wanawake, vijana na watu wenye ulemavu pamoja na wazee kwamba turasimishe biashara zetu ili tuweze kuteka hizi fursa," alisema.

Alisema makundi hayo yanapaswa kuzingatia utunzaji wa kumbukumbu za biashara, ubora, kuwa na uwezo wa kutoa huduma baada ya makubaliano na kutumia teknolojia kuingia kwenye mifumo ya kuomba zabuni.

"Mnaweza kujiunga kwenye umoja kwa muda fulani ili kuomba zabuni, hii itawasaidia kumudu zabuni kubwa. Zabuni inaweza kukuambia upeleke kiasi fulani kila wiki au mwezi na usiishiwe, umoja utatusaidia kuzalisha kwa wingi na kwa ubora ule ule. Tukiweza kufanikiwa kwenye ubora na uwezo wa kulishika soko, tutaweza kuingia kwenye masoko ya ndani na ya nje," alisema.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa TWCC, Mwajuma Hamza, alisema utafiti wa chemba hiyo wa mwaka 2021, ulibaini kwamba wanawake, vijana na makundi maalumu yanayoshinda zabuni za serikali ni chini ya asilimia mbili.

"Kwenye mpango wa B4S tunalenga kuwajengea uwezo wanawake na vijana ili wakashindane kwenye zabuni na kuonyesha matokeo. Tunataka kuona ongezeko la wanawake kutumia hii fursa. Kwa mfano, wakati fulani, Wizara ya Ujenzi ilitangaza zabuni ambayo ilitenga Sh. bilioni 80 kwa ajili ya kampuni za wanawake, ni wanawake sita tu ndio waliomba... hii inatupa picha kwamba bado tuna kazi kubwa ya kufanya," alifafanua.

Mkurugenzi Mkuu wa Trade Mark Afrika, Elibariki Shammy, alisema ili kusaidia vijana na wanawake, serikali inapaswa kulipa wazabuni kwa wakati.

"Serikali isipowalipa kwa wakati, kampuni hizi zitakufa mapema na lengo la kuwainua halitafikiwa," alisema.

Alisema serikali inapaswa kuwa na sera madhubuti ya kukuza viwanda vya ndani, ili wazawa wanaposhinda zabuni, mzunguko wa fedha ubakie kwenye uchumi nchini.

Kwa mujibu wa sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi ya Umma (PPRA), sura na 410 ya mwaka 2023 kifungu cha 64, halmashauri na ofisi zote za serikali zinapaswa kutenga bajeti yake ya ununuzi kila mwaka kwa ajili ya wazabuni wanawake, vijana na makundi maalumu.

Kanuni za sheria hiyo (PPR), ambazo zitaanza kutumia mwaka huu wa fedha 2024/2025, zinazitaka ofisi za umma kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi kwa ajili ya makundi hayo.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Mahakama yaamuru kampuni ya uchimbaji kuilipa familia mil. 150/-

**Na Ambrose Wantaigwa,**
MUSOMA

MAHAKAMA ya Rufani imeamuru kampuni ya Barrick Gold inayojihusisha na uchimbaji madini katika mgodi wa North Mara, wilayani Tarime kulipa familia moja Sh. milioni 150 kwa madhara waliyopata kutokana na shughuli za mgodi huo.

Hukumu hiyo ilitolewa baada ya rufani ya kampuni hiyo kupinga uamuzi wa kesi ya awali iliyofunguliwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania jijini Mwanza iliyotolewa uamuzi Agosti 3, 2016.

Katika kesi hiyo, Chacha Kiguha, mkewe Neema Chacha na watoto wao, Bhoke Chacha, Kiguha Chacha, Montogori Chacha na Surati Chacha walimshtaki mrufani, Meneja Mkuu, African Barrick Gold Mine Ltd, wakidai malipo ya uharibifu wa jumla wa Sh. 600,000,000.00.

Madai hayo yalitokana na uzembe wa kampuni hiyo kutenda kinyume na wajibu wa kutunza maslahi ya mlalamikaji wakati inamiliki leseni Maalum ya Uchimbaji madini (SML) katika vijiji vitano wilayani hapa kikiwamo kijiji cha wahojiwa cha Nyamwaga na kuwasababishia magonjwa.

Ilidaiwa kwamba familia hiyo ililazimika kuishi katika kipande hicho cha ardhi na kushindwa kuondoka kwa sababu ya mrufani kushindwa kulipa fidia ya haki kwa ajili ya ardhi iliyoathirika.

"Kitendo cha mshtakiwa kimesababisha kuumia kwa walalamikaji kwa idadi ya miaka kadhaa wamekuwa wakifuatilia fidia zao kwa ofisa wa mshtakiwa na kusababisha mfadhaiko mkubwa wa kiakili na uchungu," ilisema sehemu ya uamuzi huo wa awali.

Mrufani alipinga madai ya walalamikiwa Mahakama ya Rufani huku akikanusha kwamba kampuni hiyo ilishindwa kuzingatia jukumu la uangalizi na hivyo kusababisha wahojiwa kupata maradhi mbalimbali au ugonjwa wa akili kama inavyodaiwa.

Awali kampuni hiyo ilipinga hukumu ya Mahakama Kuu kwa madai, kupitia vitendo vyake vya uchimbaji walalamikaji waliathiriwa kiafya kwa kuambukizwa magonjwa ya kupumua, masikio na ngozi.

Matokeo hayo ya rufani yalitolewa mbele ya Faustine Malongo na Caroline Kivuyo ambao ni mawakili wakati mrufani na mlalamikiwa waliunganishwa kupitia mfumo wa kidijitali wa mahakama unaofahamika kama 'teleconferencing'.

Baada ya kupitia hoja zote za mrufani kwa niaba ya kampuni hiyo kuhusu hukumu iliyotolewa awali, majaji wa mahakama ya rufani wamekubaliana baadhi huku wakipinga nyingine kwa kukosekana uthibitisho.

Kutokana na uamuzi wa majaji, mjini Musoma mrufani atawajibika kulipa fidia wahojiwa kwa kusababisha kero kwao kutokana na ukiukwaji wa sheria na wajibu wa utunzaji unaosababisha j uharibifu.

"Kuzingatia asili ya uharibifu kwa mlalamikiwa na familia yake, wakiwamo watoto wadogo na ukubwa wa uzembe, mhojiwa anapaswa kupata fidia ya Sh. 25,000,000.00 kwa kila mmoja.

Mlalamikaji anaamriwa kulipa Sh. 150,000,000 pamoja na riba kwa kiwango cha mahakama cha asilimia saba kwa mwaka.

"Katika mazingira ya kesi ambapo uzembe wa kuchangia ni wanaohusika, tunaagiza kwamba kila upande ubebe gharama zake," ilieleza sehemu ya hukumu hiyo iliyotolewa Juni 14, 2024.



Mkurugenzi wa Mkuu wa Shirika la Nyumba (NHC), Hamad Abdallah (kushoto), akifafanua jambo kwa wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu mradi wa shirika hilo wa Morocco Square uliokamilika, walipotembelea, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Kampeni kudhibiti magonjwa ya wanyama kuanza

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi inakusudia kuendesha kampeni ya kutoa chanjo ya mifugo ili kuondokana na magonjwa kutoka kwa wanyama kwenda kwa binadamu.

Kampeni hiyo inafanyika baada ya serikali kutenga Sh. bilioni 28 katika mwaka wa fedha 2024/2025.

Katibu Mkuu wizara hiyo, Profesa Riziki Shemdoe, alisema hayo mjini hapa wakati akifunga mafunzo ya madaktari wa mifugo.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na kufadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Watu wa Marekani (USAID).

Profesa Shemdoe alisema madaktari waliopatiwa mafunzo hayo ndio watakaotumika kutoa huduma ya kuipatia chanjo mifugo yote hapa nchini.

"Kama wizara katika kupambana na magonjwa ya mifugo tumeamua mwaka wa fedha huu unaoanza Julai mosi tutakuwa na kampeni ya chanjo kubwa ya nchi nzima," alisema Profesa Shemdoe.

Hata hivyo, Profesa Shemdoe aliipongeza FAO kwa kazi kubwa wanayoifanya ili kuhakikisha Tanzania inakua huru na magonjwa ya wanayama kwa kuwapatia mafunzo madaktari mifugo kwa awamu tofauti katika kipindi cha muda wa miezi minne kwa mwaka huu.

"Serikali tumetenga Sh. bilioni 28 kwa ajili ya kazi hii na tunatumai tukifanikiwa kupata wadau wengine wakutuongezea fedha ni jambo la heri," alisema Profesa Shemdoe.

Mwakilishi Mkazi wa FAO nchini, Nyabenyi Tipo Tito alitumia nafasi hiyo kupongeza uratibu wa Serikali ya Tanzania katika Programu ya Utoaji wa Taarifa na Ufuatiliaji wa Magonjwa (ISAVET)- (In-Service Applied Veterinary Epidemiology Training).

Nyabenyi alisema Programu ya ISAVET inasaidia kupunguza umaskini na njaa duniani kwa kuboresha uchumi wa jamii vijijini, na usalama wa chakula sio tu kulinda afya ya binadamu lakini pia kupunguza upotevu wa wanyama.

Mkurugenzi wa huduma ya mifugo wa wizara hiyo, Dk. Benezeti Malinda alisema mafunzo hayo ya awamu ya nne kwa maofisa mifugo nchini ni ya kuwawezesha kutambua na kutibu magonjwa ya mifugo ili kuboresha ufugaji wenye tija na kulinda soko la mifugo kimataifa.

Alisema hali ya chanjo chini ipo vizuri na kwamba Tanzania ina viwanda vitatu vya kuzalisha chanjo ambapo kimoja ni cha Serikali kilichopo Kibaha, mkoani Pwani kinacho zalisha aina saba za chanjo.

Dk. Malinda alisema serikali kwa kushrikiana na wadau wengine ikiwamo FAO wameweza kwa kiwango kikubwa kudhibiti ugonjwa wa sotoka kwa wanyama wadogo ikiwamo kondoo na mbuzi.

Alisema katika kufikia hatua kuutokomeza ugonjwa huo, serikali inaweza kuandaa nyaraka kwa ajili ya kuiwasilisha Shirika la Mifugo Duniani ili kuomba kibali cha kutangazwa Tanzania ni huru kutokea kwa ugonjwa wa Sotoka.

## Kijiji cha Bugando chaanza kunufaika ujenzi wa zahanati

**Na Yusuph Digossi,** MAGU

ZAIDI ya wananchi 2000 wa Kijiji cha Bugando na vijiji vya jirani Kata ya Chabula, wilayani Magu, wameanza kunufaika na mradi wa ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Bugando iliyojengwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF) kwa kushirikiana na wananchi waliochangia asilimia 10 ya mchango wa jamii.

Zahanati hiyo imejengwa na TASAF kwa gharama za Sh. milioni 93 na kukamilika ikiwa na vifaa vyote pamoja na dawa.

Hata hivyo, miundombinu mingine ya kuboresha utoaji wa huduma inaendelea kukamilishwa ikiwamo nyumba ya kuishi watumishi wa afya wa zahanati hiyo ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 95 huku wodi ya wazazi ikiendelea kujengwa.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa zahanati hiyo iliyozinduliwa na Mbunge wa Jimbo la Magu, Boniventura Kiswaga, Mwenyekiti wa Kijiji cha Bugando, Charles Kasuka, alisema kukamilika kwa zahanati hiyo kutawaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya katika kata za jirani.

"Tunaishukuru sana serikali kupitia TASAF kwa kutujengea zahanati hii kwa sababu kilikua ni kilio chetu cha muda mrefu, wananchi walikua wanatembea umbali mrefu kufuata huduma za afya hasa kinamama na watoto. Hivyo tunashukuru sana serikali kwa kutujengea zahanati hii amesema."

Mbunge wa Jimbo la Magu, Kiswaga ameishukuru serikali inayoongozwa na Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Magu ikiwamo ujenzi wa zahanati ya kijiji cha Bugando.

Alisema serikali itaendelea kuboresha sekta ya afya kwa kuendelea kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na ununuzi wa vifaa tiba ili kuendelea kupeleka huduma za afya kwa wananchi kuanzia ngazi za chini.

Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Magu, Eusebius Chanjali, amewataka wananchi wa Kijiji cha Bugando kutumia zahanati hiyo kutatua changamoto za kiafya huku akiwaomba kutoa ushirikiano wa watumishi wa zahanati hiyo ili watekeleze majukumu yao ya kuwahudumia wananchi bila changamoto yoyote.

Naye Mratibu wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Wilaya ya Magu, Daniel Sanyenge, amesema serikali imejenga zahanati hiyo kutokana na uhitaji mkubwa kwa wakazi wa maeneo hayo ambao wanatembea umbali huo kwenda kata jirani kufuata huduma za afya.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Magu, Mohamed Ramadhani aliwaomba wananchi kuendelea kushiriki kikamilifu katika ujenzi na ulinzi wa miradi inayojengwa na serikali ili ilite tija iliyokusudiwa ya kutoa huduma.



# EWURA yaelekeza nguvu matumizi ya vinasaba

Na Godfrey Mushi, MOSHI

MAMLAKA ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA), baada ya kufanikiwa kupunguza uchakachuaji wa mafuta ya dizeli na petroli nchini, sasa imeweka nguvu kubwa katika matumizi ya vinasaba ili kuzuia udanganyifu wa wafanyabiashara wa mafuta.

EWURA imepunguza uchakachuaji huo wa mafuta kutoka asilimia 78 mwaka wa 2007 hadi asilimia nne ya sasa.

Akizungumza na wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu waliokutana katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Meneja wa Kanda ya Kaskazini EWURA mwishoni mwa wiki, Lorivii Long'idu, alisema ili kuimarisha mpango huo, EWURA ilianzisha programu maalum ya kuweka vinasaba hivyo kwenye nishati ya mafuta ili kudhibiti uchakachuaji na uhifadhi wa mafuta.

Alisema mpango huo umeleta matumaini kwa kuwezesha kuweka ushindani wa mazingira ya biashara miongoni mwa wafanyabiashara wa mafuta.

Kutokana na mpango huo kuanzishwa, amewasihi wananchi kutosita kupeleka malalamiko yao kwa mamlaka hiyo ili kushughulikiwa mapema kwa kuwa wanayo haki ya kisheria kufanya hivyo.

"Kwenye kutolewa huduma ni nadra kukosa watu wenye malalamiko ya hapa na pale. Nitoe rai kwa wananchi wote wenye malalamiko ya aina yoyote, kuyawasilisha kwetu maana ni moja wapo ya majukumu yetu kuyashughulikia ili wananchi waendelee kupata hudma nzuri na bora", alisema.

Aidha, Long'idu, ameeleza kuwa mamlaka hiyo inapambana kuhakikisha walaji wanapata huduma zilizo salama.

Vilevile, alieleza kuwa mamlaka hiyo imeandaa mazingira mazuri na yenye masharti nafuu, ili kuvutia wawekezaji wajitokeze kwa wingi kuwekeza kwenye eneo la nishati safi, hasa maeneo ya vijijini.

Kuhusu mafunzo hayo, Long'idu, alisema kuwa yamelenga kutoa elimu kwa wanafunzi vya vyuo vya elimu ya juu ili wapate kujua shughuli zinazofanywa na EWURA na umuhimu wa kuwepo kwa mamlaka hiyo.

Akizungumzia kuhusu changamoto ambazo mamlaka hiyo inakumbana nazo wakati wa utekelezaji wa majukumu yake, Long'idu, alisema ni pamoja na mamlaka hiyo kuchelewa kutoa leseni kwa wanaoshika na kutoa huduma mbalimbali.

**EWURA imepunguza uchakachuaji huo wa mafuta kutoka asilimia 78 mwaka wa 2007 hadi asilimia nne ya sasa.**

# CCM yaanza kuwapika vijana kuelekea uchaguzi

Na Mary Mosha, MOSHI

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimeanza kutengeneza vijana maalum watakaobeba dhamana ya kutetea viti vyake vya wenyeviti wa serikali za mitaa 60 katika Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro ili isiangukie mikono ya wapinzani.

Jana, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Vijana Chama Cha Mapinduzi, Manispaa ya Moshi (UVCCM), Sadath Ndibalema, alisema vijana hao wamepewa mafunzo mbalimbali yakiwemo ya ukakamavu, uzalendo, kutetea chama hicho na kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali kwenye uchaguzi huo.

Alisema vijana 300 waliibuliwa katika kila mitaa, waliwekwa kambini kwa siku tano kupigwa msasa wa namna watakavyokabiliana na hoja za wapinzani na kushinda uchaguzi ujao wa mitaa, vijiji na vitongoji, unaotarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu.

Ndibalema alisema kambi hiyo iliwekwa katika Chuo cha Maendeleo cha Singa, kilichopo Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Vijana hawa wamepata mafunzo ya aina nyingi ikiwemo kufundishwa uzalendo, kutetea chama chao na kusimamia misingi ya sheria, taratibu na kanuni za nchi katika kuelekea kwenye chaguzi, lengo ni kupata viongozi bora na wenye tija kwa jamii yetu watakaoleta tija,"alisema Ndibalema.

Akifunga mafunzo hayo, Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Patrick Boisafi, aliwataka vijana kuzingatia muda kwenye kila jambo, huku akisisitiza kutoridhishwa na taalumu zao.

"Vijana, punguzeni kupoteza muda kwa mambo yasiyo na tisha na kisha kujiita wasomi, ili uwe msomi mwenye tija ni lazima uweze kutafsiri ulichosoma kwa vitendo na kilete tija.

Vijana wengi mnalalamika hakuna ajira lakini nyinyi hamjitumi kuwa wabunifu katika kutatua matatizo ya jamii na pia wengi wenu siyo waaminifu, hii inafanya vijana kutoaminiwa kwenye kila eneo wanalofanya kazi hii siyo dalili nzuri kwa kizazi kijacho. Mnapaswa kujitathimini " alisema Boisafi.

Mwenyekiti wa UVCCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Ivan Moshi, alisema kuwa watu ambao watakifanya chama kishinda kwa urahisi katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 ni viongozi wa dola waliochaguliwa mwaka 2020.

Alisema kuwa baadhi ya madiwani wamekuwa hawafanyi mikutano ya hadhara ya wananchi lakini wamekuwa wakisuguana na wabunge, ambapo kila mmoja amekuwa akimtupia lawama mwenzake na kukiomba chama kuhakikisha kila kiongozi anatimiza wajibu wake.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Moshi, Zephania Sumaye, alisema CCM kinahitaji vijana jeuri na wenye akili ya kuhoji jambo na kuweza kulitetea mbele ya jamii.

Sumaye alisema kesho ya Tanzania imewekwa katika mabega ya vijana na siyo rasilimali zilizopo ambapo kambi hizo zinasaidia vijana kupata elimu.

# Watoto 245 wabainika na utapiamlo mkali Manyara

Na Jaliwason Jasson, MANYARA

WATOTO 245 kutoka maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Manyara, wamebainika wanakabiliwa na utapiamlo mkali, ambao unatishia ukuaji na ustawi wao kiafya.

Kwa mujibu wa Ofisa Lishe wa Mkoa huo, January Dalushi, waliogunduliwa ni watoto chini ya miaka mitano.

Alisema tayari serikali imechukua hatua za makusudi za kukabiliana na hali hiyo, kwa kuwapa tiba watoto 128 kati yao, sawa na asilimia 88.

Dalushi alisema walipoteza maisha kwa kipindi hicho ni watoto watano na watoto 12 walipotea kwenye matibabu ya ufuatiliaji.

Aidha, alisema hali ya lishe kwa mkoa huo inaendelea kuimarika ambapo kwa matokeo ya utafiti wa mwaka 2022 udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ni asilimia 32 kutoka asilimia 36 mwaka 2015.

Kadhalika alisema ukondefu kwa watoto chini ya miaka mitano ni asilimia 4.7, uzito pungufu ni asilimia 18.9, uzito uliozidi ni asilimia 2.8, upungufu wa damu asilimia 45.7 na unyonyeshaji maziwa ya mama pekee kwa miezi sita ni asilimia 55.2.

Akizungumzia mkakati wa serikali, Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Maryam Muhaji, alisema ili kukabiliana na tatizo hilo, ofisi yake inachunguza kila mwezi watumishi ambao hawawajibiki kusimamia huduma za lishe.

Muhaji, alisema haoni sababu za mkoa huo kuwa na udumavu kutokana na uwepo wa chakula.

"Utendaji kazi wangu napimwa kwenye lishe pia hata kama ni Jumapili niko tayari kuja kujadili masuala ya lishe,"alisema Muhaji


Nipashe ilipata fursa ya kuongea na wananchi juu ya uelewa wao wa utapiamlo mkali kwa watoto, mkazi wa Mtaa wa Komoto, Rehema Paschal alisema bado hajui utapiamlo mkali unafananaje.

Paschal, aliiomba serikali kuongeza juhudi za utoaji wa elimu kwa wananchi ili wawe na uelewa wa namna ya kudhibiti utapiamlo mkali na udumavu kwa watoto.

Mkazi wa Kijiji cha Daghailoy, John Akonay, alisema utapiamlo mkali anafikiri ni wale watoto waliokonda na matumbo yao yamejaa.

Alisema ili kutibu tatizo hilo ni vizuri wataalamu wa lishe wapige kambi maeneo ya vijijini na kutoa elimu ya namna ya kuandaa vyakula vya watoto ambavyo vinapatikana maeneo hayo.



# Kanisa ladaiwa kuzuia wajawazito kujifungulia hospitali, DC alifunga

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro, amelifunga Kanisa la Church Of God, lililopo katika Kijiji cha Mendo, wilayani Shinyanga kwa madai ya kuzuia wajawazito wanaosali kanisani hapo wasiende kujifungulia hospitali, badala yake watazalishwa na wahudumu wa kanisani hapo.

Mtatiro alichukua uamuzi huo juzi, alipofanya mkutano wa hadhara wa kusilikiza kero za wananchi wa Kijiji hicho na kupokea malalamiko kuwa kanisa hilo limekuwa kero kwao kwa kutoa mafundisho kinyume ikiwemo kuzalisha wajawazito na kusababisha vifo vya watoto.

Mmoja wa wananchi wa kijiji hicho, Robert Paulo, alisema kanisa hilo limekuwa kero kijijini hapo kwa kutoa mafundisho ya upotoshaji ikiwamo kuzuia wajawazito kwenda kliniki na kujifungulia hospitali, bali huduma zote watapewa kanisani hapo.

"Mkuu wa Wilaya Kanisa hili ni shida, hatulitaki hapa kijijini na mchungaji wao waondoke, wameshasababisha vifo vya watoto watatu sasa, kutokana na kuwazalisha wenyewe wakiwa hawana ujuzi wowote," alisema Paulo.

Mwananchi mwingine, Wilelwa Mwinamila, alisema kanisa hilo limekuwa likizuia hata watoto kwenda kupatiwa chanjo, huku wazazi pia wakipigwa marufuku kuwapatia watoto wao majina ya ukoo.

Mmoja wa wanawake ambaye mtoto wake alifariki wakati akijifungua kanisani hapo, Neema Juma akisimulia namna mkasa ulivyomkuta alisema ilikuwa ni siku ya Jumapili alijisikia tumbo kuuma, ndipo mama yake akamwambia ampeleke hospitali.

Alisema lakini yeye aligoma kwa madai kwamba walishaambiwa na mchungaji wao watazalishwa kanisani.

Alisema alipofika Kknisani alianza kuombewa na kwamba muda kidogo alijisikia nafuu tumbo kuacha kuuma, ndipo akaomba akapunzike na alipoilaza kidogo alisikia kama mtoto anaanza kutoka, ndipo wahudumu wa kanisa wakaanza kumzalisha na hatimaye mtoto alifariki dunia.

"Huu ni uzao wangu wa kwanza sikuwa na uelewa wowote kuhusu uchungu, wala sina elimu ya uzazi sababu sijawahi kuhudhuria lliniki kutokana na kuzuiwa kwenda hospitali na mchungaji wetu," alisema na kuongeza:

"Baada ya mtoto kufariki na mimi kuwa katika hali mbaya alikuja baba yangu na kuamuru nipelekwe hospitali na sasa naendelea vizuri," alisema Neema.

Mchungaji wa Kanisa hilo, Andrew Mussa, alikana tuhuma hizo na kusema kwamba hawajawahi kuwazuia wajawazito wasiende kliniki wala kujifungua hospitali wala kuwazalisha kanisani hapo.

Baada ya kupokea malalamiko hayo, Mtatiro aliagiza kwamba Kanisa hilo lifungwe kwa muda, hadi pale serikali itakapokamilisha taratibu zingine na kujiridhisha hali ya amani na usalama inarejea kwa wananchi.

"Siwezi kuwa na nyumba ya ibada wilayani kwangu ambayo inafanya kazi ya kuzalisha kinamama na hata kusababisha vifo vya watoto, kwa hiyo kanisa hili tunalifunga rasmi na halafu tutaendelea na taratibu zingine," alisema Mtatiro.

Aidha, aliwataka wajawazito waendee kujifungulia kwenye vituo vya huduma za afya sehemu ambazo ni salama, huku akitoa wito kwa viongozi wa madhebu ya kidini kuwapatia mafundisho sahihi waumini wao.

# Auawa kwa kukatwa mapanga na watu wasiojulikana

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKAZI wa Kitongoji cha Ipyagula katika Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, Joyce Masasila (57) amefariki dunia kwa kupigwa mapanga sehemu mbalimbali za mwili wake na watu wasiofahamika.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Kennedy Mgani, amethibitisha kutokea kwa tukilo hilo akisema lilitokea Juni 23 mwaka huu majira ya saa mbili usiku.

Alisema Joyce alifikwa na mkasa huo wakati akitoka dukani kufanya manunuzi ya mahitaji ya familia yake, huku akiwa ameambatana na mtoto pamoja na mjukuu wake.

Alisema Joyce alipoteza maisha akiwa katika Hospitali ya Manispaa ya Kahama wakati akipatiwa matibabu na upelelezi unaendelea kuwabaini waliohusika na tukio hilo.

Aidha, Kamanda Mgani aliwataka wananchi kuacha tabia ya kujichukulia sheria mkononi kwa kufanya matukio ya kikatili na badala yake kama mtu anachangamoto au kudaiana ni vyema wakafikishana katika vyombo vya sheria kutafuta mhafaka.

Wakisimulia tukio hilo, mtoto wa marehemu Ibrahim Kitinga, alisema ilikuwa majira ya saa mbili usiku wakielekea nyumbani baada ya kutoka dukani, walikutana na watu wawili na mmoja alikuwa amefiicha panga kwa nyuma na alipogeuka mama yake alimshambulia katika paji la uso.

Alisema alimvuta mama yake ili wakimbie lakini walizidi kuongezeka washambuliaji na kuwazidi nguvu, walipokuwa wakimpiga panga mama yake alikuwa akikinga au kujihami kwa kuweka mikono.

Ibrahim alisema alipiga kelele ya kuomba msaada kwa wakati huo lakini hakuna na hata jirani aliyejitokeza kuwasaidia.

"Nasikia maumivu makubwa sana moyoni mwangu, nimeshuhudia kifo cha mama yangu kwa macho yangu, wakati wanamkata panga alikuwa akijihami kwa kuweka mikono yake, ili wasimkate sehemu ya shingoni, licha ya kumjeruhi kwenye paji lake la uso, ninaimani serikali itawabaini walihusika na tukio hili," alisema Ibrahim.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kagongwa, Michael Shija, alisema alipata taarifa ya tukio hilo Juni 23 majira ya saa mbili usiku na sasa anashirikiana na Jeshi la Polisi kuwabaini waliohusika na tukio hilo.


## MNADA WA HADHARA/NOTISI

Dalali tajwa hapo chini tunatangazia umma kuwa kutakuwepo na mnada wa hadhara wa kuuza dhamana ya mdaiwa kama ilivyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Mnada utaendeshwa kwa idhini tuliyopewa na Tujijenge Tanzania Financial Service Ltd kama ilivyotangazwa gazetini,

Pia tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) ya kulipa deni kwa mdaiwa, vinginevyo tutafanya mnada wa hadhara kama ratiba inavyoonyesha gazetini

| Mdaiwa | Dhamana/ Mahali ilipo | Tarehe ya mnada | Dalali |
|---|---|---|---|
| MRBM GROUP COMPANY LIMITED | Gari T.408 EBH TOYOTA LAND CRUISER - Dalali Yard | 29/07/2024 | SEPCO Debt Collections & Auctioneering Co. Ltd |

**Masharti Mengine:**
Mnada utafanyika mahali dhamana ilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14, akishindwa kulipa 25% iliyolipwa hairudishwi na mnada utarudiwa tena. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:**
**SEPCO: 0715683777**
**Tujijenge (T) Financial Services Ltd: 0718068335**



**KATIKA BARAZA LA ARDHI NYUMBA NA MAKAZI**
**SONGEA LILILOKO SONGEA**

**MAOMBOI NAMBA 46/2024**
**RICHARD MBUNDA..................MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**FURAHA HAULE .................. MJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

Mjibu maombi unaarifiwa kuwa muombaji amefungua shauri la mgogoro wa ardhi dhidi yako.
Hivyo basi unatakiwa kufika shaurini bila kukosa binafsi au wakili wako, au wote kwa pamoja siku ya tarehe **03/07/2024 saa 2:30** asubuhi. Shauri linakuja kwa ajili ya kutajwa.
Kumbuka pia kushindwa kwako kufika shaurini kutapelekea baraza hili kusikiliza shauri hili bila kujali uwepo wako
Imetolewa leo nami na muhuri wa Baraza hii leo tarehe 26/6/2024



**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MTWARA**
**MKOA WA MTWARA**
**MAOMBI NA 31/2023**
**ELINURU EDWARD JUMANNE...MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**QUEEN ELIZABETH LTD......MJIBU MAOMBI NA 1**
**WICOM FINANCE LTD............MJIBU MAOMBI NA 2**
**FAUSTINE SAMWEL BAYAGA..MJIBU MAOMBI NA 3**
**D AND G AUCTION MART LTD...MJIBU MAOMBI NA 4**

**KUITWA SHAURINI**
D&G AUCTION MART LTD POPOTE ULIPO, FAHAMU kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 04, july, 2024 saa 02:30 asubuhi.
UNAAMRIWA kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la Baraza idara ya Ardhi Manispaa ya Mtwara siku hiyo bila kukosa, wewe au mwakilishi wako kisheria . Hati ya madai pamoja na vielelezo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masijala ya Baraza.
FAHAMU KWAMBA Kushindwa kuhudhuria barazani siku hiyo shauri litapangiwa kusikilizwa upande mmoja na kuamuriwa dhidi yako
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 21 june, 2024

NGUKULIKE,N.O
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MTWARA.



**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA MTWARA**
**MKOA WA MTWARA**
**MAOMBI NA 45/2023**
**HAMISI RASHIDI MNALI......MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**SIJALI MHONDOGWA T/A NGADU SEA FOOD ENTERPRISES.........MJIBU MAOMBI NA 1**

**KUITWA SHAURINI**
SIJALI MHONDOGWA T/A NGADU SEA FOOD ENTERPRISES, POPOTE ULIPO, FAHAMU kwamba shauri hili limepangwa kutajwa tarehe 01 , July 2024 saa 02: 30 asubuhi.
UNAAMRIWA kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la Baraza Idara ya Ardhi Manispaa ya Mtwara siku hiyo bila kukosa, wewe au mwakilishi wako kisheria. Hati ya madai pamoja na vielelzo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masjala ya Baraza.
FAHAMU KWAMBA kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litapangiwa kusikilizwa upande mmoja na kuamriwa dhidi yako.
Amri hii imetolewa kwa mkono wanu na muhuri wa Baraza leo tarehe 17 Mei, 2024

NGUKULIKE,N.O
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W) MTWARA.


# Watumishi 2 wa afya wafa ajali ya bodaboda wakipanda 'mshikaki'

**Na Elizabeth John,** WANG'ING'OMBE

WATUMISHI wawili wa afya katika Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, wamefariki dunia na mmoja kujeruhiwa baada ya bodaboda waliyokuwa wamepanda wakitoka kazini kugongana na gari dogo.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu jana, Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi, Ally Kitumbu, alisema watumishi hao walikuwa wamepanda pikipiki kwa mtindo wa 'mshikaki' wakielekea nyumbani, mwishoni mwa wiki.

Pikipiki hiyo ni yenye namba za usajili MC 894 DTU na waligongwa na gari yenye namba za usajili T107 DQN.

Waliofariki ni Ofisa Muuguzi Msaidizi Daraja la Pili, Raufu Samu (34) aliyekuwa dereva na Ofisa Tabibu Meno Daraja la Pili, Patrick Chaula (38) huku Ofisa Tabibu Daraja la Pili Asia Chitiku (28), akijeruhiwa.

Alisema ajali hiyo ilitokea Juni 28, majira ya saa 1:15 jioni katika Kijiji cha Igwachanya na maofisa hao wawili walifariki wakati wanaendelea na matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Njombe.

Kamanda Kitumbu alisema chanzo cha ajali hiyo ni dereva wa gari hilo kutojali watumiaji wengine wa barabara, huku akieleza kuwa majeruhi alihamishiwa katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kwa matibabu zaidi.

Alisema Jeshi la Polisi linamsaka dereva wa gari hilo, Noah Kipanga, mkazi wa Makambako ambaye alikimbia baada ya ajali hiyo kutokea.

"Baada ya tukio hilo huyu dereva alitokomea kusiko julikana, lakini juhudi za kumtafuta bado zinaendelea," alisema.

Akizungumza wakati wa kuaga miili ya marehemu hao, Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka alisema halmashauri hiyo imepoteza watumishi wachanga na mahiri kwenye kada ya afya.

Aidha, alisema vifo hivyo vimesababisha maumivu kwa serikali, jamii, watoto, mke na wazazi kwa sababu watumishi hao waliajiriwa 2022/23.

"Ni watumishi ambao wana mwaka mmoja kazini unaweza kusema ni ua la Krismasi lililonyauka mwaka mpya na uchungu wake unauona kwa tulioko hapa, mwaka mmoja mzazi anapokea mtoto akiwa kwenye jeneza sio jambo jepesi ni jambo gumu," alisema Mtaka.

Aliiagiza halmashauri hiyo kushughulikia na kusimamia stahiki zote za kiutumishi za marehemu hao, ili familia zao zisihangaike.

"Isianze tena mzazi au mjane kuja kupanga foleni hapa kufuatilia stahiki za mwenza au za mtoto kwa sababu nimeona kwenye ofisi sisi wenyewe watumishi hatujaliani, simamieni maana yake kuna familia zetu tunajuana mkifika kule wanaanza kuulizana walifunga ndoa lini," alisema.

"Hakuna mtu anayejua kwamba kuna watoto wanahitaji kusoma kwa hiyo tunakuwa na ujinga mwingi kwenye misiba halafu mwisho wa siku anabaki mama na watoto wake," alisema.

Paroko kutoka Kata ya Igwachanya, Padri Clement Mgohele, alisema muhimu katika binadamu ni roho yake ambayo inaunganika moja kwa moja na Mwenyezi Mungu.

"Ikiwa hapa duniani roho hii ni nyumba yake ni mwili wako huo na maandiko yametuambia nyumba hii ya duniani utake usitake itabomoka ndivyo wenzetu Patriki na Raufu nyumba yao ya hapa duniani mwili umebomoka," alisema Mgohele.

Mkuu wa Wilaya ya Wang'ing'ombe, Claudia Kitta, alisema baada ya ajali hiyo madaktari na manesi walijitahidi kuokoa maisha ya wenzao.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Wanging'ombe, Agnetha Mpangile alisema halmashauri imepata pigo kwa sababu ni kipindi wanachohitaji watumishi wengi, lakini wanavyopungua ni pengo kubwa.

Nipashe
# Spotika



WANASOKA WA5 MATAJIRI AFRIKA WENYE MIOYO YA KUSAIDIA JAMII UK. 12-13



# KLABU 5 ZINAZOWANIA HUDUMA YA KIMMICH

**MUNICH,** Ujerumani

JOSHUA Kimmich angependa kujiunga na klabu moja kati ya Arsenal, Liverpool, Manchester City, Barcelona au Real Madrid, kulingana na ripoti, na kuondoka kwake Bayern Munich 'kuna uwezekano mkubwa'.

Mkataba wa Kimmich katika Uwanja wa Allianz Arena unatarajiwa kumalizika 2025 na mazungumzo kuhusu mustakabali wake hayajapangwa hadi baada ya kampeni yake ya Euro 2024 akiwa na Ujerumani.

Sky Sport Germany wanaripoti kwamba wakati Kimmich anajiandaa kuingia mwaka wa mwisho wa mkataba wake na mustakabali wake ambao haujaamuliwa, Bayern wako tayari kumuuza msimu huu wa majira ya joto ili kurudisha ada ya aina yoyote ya uhamisho na hakuna uwezekano kuwa atakuwa katika klabu hiyo. muda mrefu zaidi.

Arsenal, Liverpool, City, Barcelona na Madrid basi zimetajwa kuwa klabu tano ambazo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, angefikiria kujiunga nazo.



Nyota wa Bayern Munich, Joshua Kimmich, akiwa na watoto wenye ndoto za kufikia mafanikio yake katika soka.

Kinyume cha kuvutia kuhusu hali ya Kimmich ni kwamba wakati bado anashauriwa na wataalamu, hana wakala kwa sasa na anafanya mazungumzo mwenyewe. Klabu hizo zinazovutiwa na huduma yake, zitalazimika kuwasiliana naye moja kwa moja ikiwa zinataka kujadili uhamisho.

Hali ya Kimmich kama mmoja wa wachezaji nyota kadhaa wa Bayern na mkataba wao unaomalizika 2025, ilisababisha mustakabali wake kutiliwa shaka kwa muda mwingi wa msimu uliopita. Beki wa kushoto Alphonso Davies vile vile amekuwa akihusishwa pakubwa na mpango wa kuondoka, huku Real Madrid wakiwa na nia ya kumpeleka Mcanada huyo Santiago Bernabeu.

Bayern walipoteza msururu wao kwenye Bundesliga na kumaliza nafasi ya tatu nyuma ya washindi wa taji, Bayer Leverkusen na Stuttgart iliyo nafasi ya pili, huku wakitupwa nje ya DFP Pokal na timu ya daraja la tatu Saarbrucken.

Katika Ligi ya Mabingwa, The Bavarians walikubali kufungwa mara mbili mwisho kwenye mechi ya mkondo wa pili wa nusu fainali dhidi ya washindi wa mwisho Madrid, ambao waliwaondoa katika mazingira ya ukatili.

Kabla ya msimu wa 2024/25, Bayern wamemteua Vincent Kompany kama kocha wao mkuu, akichukua nafasi ya Thomas Tuchel. Mazungumzo yalifanyika na Ralf Rangnick na meneja wa zamani Julian Nagelsmann kabla ya kumgeukia Kompany, ambaye alishushwa daraja na Burnley msimu uliopita miezi 12 baada ya kunyanyua taji la ubingwa.

## ISIKUPITE

CRISTIANO Ronaldo alikuwa mfungaji bora wa pamoja kwenye Euro 2020 na macho yote yalikuwa kwa yeye kama mkufunzi wa timu ya Ureno nchini Ujerumani, lakini mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 39, hakufanikiwa kufunga bao lolote katika hatua ya makundi - hii ikiwa ni mara ya kwanza kwake katika michuano ya Euro au Kombe la Dunia, hata hivyo ana mashuti 12 hadi sasa kwenye Euro 2024 - zaidi ya mchezaji mwingine yeyote.



Time

# WANASOKA WA5 MATAJIRI AFRIKA WENYE MIOYO YA KUSAIDIA JAMII


MO SALAH

**LONDON,** England

SOKA ni mchezo pendwa duniani, unatajwa kufuatiliwa na watu zaidi ya bilioni nne, ukiingiza mabilioni ya dola kwa wachezaji na watu wengine wanaoshughulika na soka. Ukitaja wanamichezo wanaolipwa pesa nyingi duniani, wacheza soka ni miongoni mwao.

**Ukiacha malipo ya mishahara wachezaji wa soka wengi wanapata fedha kutokana na matangazo ya kibiashara na haki ya kutumika kwa sura zao.**

Ukweli ni miongoni mwa binadamu wanaoishi kifahari ikiwamo kununua majumba mazuri, magari mazuri ya kifahari, ndege na anasa zingine.

Kuwa na fedha ni jambo moja, kuwa na moyo wa kurudisha ulichovuna kwa jamii ni jambo lingine. Wapo wachezaji wa sasa na waliostaafu wenye mioyo ya kutumia fedha zao na umaarufu wao kusaidia jamii.

Cristiano Ronaldo, Mesut Ozil, David Beckham, Lionel Messi, Riyad Karim Mahrez , Mario Balotelli, Yakubu Ayegbeni, Neymar na Marcus Rashford ni miongoni mwa wanasoka wachache duniani wenye mioyo ya kipekee ya kusaidia jamii kwenye maeneo tofauti tofauti. Kwa bara la Afrika wafuatao ni wanasoka watano wanaotajwa kuwa na mioyo ya kipekeee ya kusaidia jamii zao.

### 1: Mohamed Salah

Walemavu ni miongoni mwa makundi yanayosaidiwa sana na Mo Salah

Salah ni mmoja kati ya wachezaji bora duniani, akiwa anapokea mshahara mkubwa zaidi katika klabu yake ya Liverpool akipokea zaidi ya dola milioni 14 kwa mwaka. Kama ilivyo kwa nyota mwenzake wa Liverpool, Sadio Mane, pia hajasahau alipotoka, nchini Misri. Mo Salah alitoa maelfu ya mitungi ya oxygen kwenye hospitali za Misri kwa ajili ya kukabiliana na janga la corona.

Mwaka 2019, alichangia dola za Kimarekani milioni tatu sawa na Sh. bilioni 8.2 za Tanzania, kwenye taasisi ya kansa nchini Misri, ili ifanye ukarabati wa miundombinu yake baada ya kushambuliwa na magaidi.

Mwaka 2018, alitumia dola karibu nusu milioni kusaidia kununua eneo kubwa la kujenga mradi wa maji katika kijiji chake cha Nagrig. Mbali na hiyo ana miradi mingi ya kusaidia watu katika kijiji hicho na Misri kwa ujumla ikiwamo kuanzisha Taasisi ya Misaada ya Al-Azhar na kituo kikubwa cha huduma za magari ya wagonjwa wa dharura (Ambulance).

### 2: Samuel Eto'o

Huyu anatajwa kama mchezaji wa muda wote wa Afrika. Mshambuliaji huyu wa zamani wa Timu ya Taifa ya Cameroon na klabu kubwa kama Barcelona, Chelsea na Inter Milan, mbali na kuonyesha dunia uwezo wake wa kusakata kabumbu uwanjani, anaonyesha utu wake pia nje ya uwanja.

Amejielekeza zaidi kutimiza ndoto za watoto na vijana wengi kwenye maisha yao, mbali na kusaidia huduma za msingi kama malazi na chakula, amekuwa akiwasaidia pia kupitia kuwafadhili kwenye masomo yao. Ameshiriki kwenye miradi mingi ya kusaidia miundombinu ya afya barani Afrika.

### 3: Sadio Mane

Mchezaji bora wa Afrika mwaka 2019, ni miongoni mwa wachezaji wanaolipwa mshahara mkubwa zaidi akipokea zaidi ya dola milioni 10 kwa mwaka. Anatajwa kama mwanasoka mwenye utu zaidi kwa sasa. Utu wake ukijengwa zaidi na alivyoshikilia dini kwa imani yake ya kiislamu.

Hatumii fedha yake yoyote kwa ajili ya starehe, anaishi kama mtu mwenye pesa, lakini si kifahari kama wachezaji wengine wa Afrika. Pesa yake nyingi anairejesha nyumbani kwao Senegal na familia yake.

"Kwa nini nitake kununua magari 10 ya Ferraris, saa 20 sa almasi au ndege mbili? Hivi vyote vitanisaidiaje mie na dunia? Aliwahi kunukuliwa hivi karibuni akisema

"Nimeishi maisha magumu ya kimasikini, nimecheza mpira bila viatu utotoni, sijasoma mie, lakini leo navuna fedha nyingi , asante soka, sasa naweza kusaidia watu wangu."

Anaishi katika maneno yake, ukiacha michango ya kawaida anayotoa katika maeneo mengi ya Afrika, Mane amejenga shule kijijini kwao, Bambuli Senegal, amejenga hospitali kubwa na msikiti mkubwa wa kuabudia jamii yake

### 4: Didier Drogba

Ukiwataja wanasoka waliowika zaidi kwenye soka Afrika katika miaka ya hivi karibuni, huwezi kumuacha mshambuliaji huyu wa zamani wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ivory Coast. Ni gwiji aliyeanzisha taasisi yake ya Didier Drogba Foundation, ambayo imejenga hospitali kadhaa, shule na vituo vya kusaidia watoto yatima.

Moyo wake wa huruma unakumbukwa zaidi mwaka 2007 alipomaliza vita ya wenyewe kwa wenyewe nchini mwake iliyodumu kwa zaidi ya miaka mitano. Moyo wake wa kusaidia hauishii tu nchini kwake, zaidi ya nchi 10

### 5: Nwankwo Kanu

Mashabiki wa Nigeria na Arsenal wanamfahamu sana huyu, akiwa sehemu ya kikosi cha Arsenal kilichoshinda taji la Ligi Kuu England msimu wa 2003/2004 bila kupoteza hata mchezo mmoja 'Invincibles'.

Kanu aliyewahi kutwaa tuzo ya mchezaji bora wa Afrika mara mbili, anatajwa kuwa na utajiri wa dola milioni tisa, uliotokana na soka.

Ameamua kurejesha utajiri wake kwa jamii kwa kuanzisha moja ya hospitali kubwa ya moyo Afrika na kurejesha tabasamu kwa Waafrika wengi. Kanu Heart Foundation ilianzishwa mwaka 2000 akiwa bado mchezaji wa Arsenal baada ya kupata tatizo la moyo, akiwa mchezaji. Mpaka sasa maelfu ya watoto katika nchi za Afrika Magharibi wamenufaika na mradi huo.

## Nukuu

"Kwa nini nitake kununua magari 10 ya Ferraris, saa 20 za almasi au ndege mbili? Hivi vyote vitanisaidiaje mie na dunia?Nimeishi maisha magumu ya kimasikini, nimecheza mpira bila viatu utotoni, mimi sijasoma, lakini leo navuna fedha nyingi, asante soka, sasa naweza kusaidia watu wangu," **mshambuliaji wa Al Nassr na Senegal, Sadio Mane**



"Sidhani kama nimeshuhudia, katika maisha yangu, timu mbaya zaidi ya Italia kuliko hii," **mshambuliaji wa zamani wa England, Gary Lineker, baada ya kuwashuhudia mabingwa watetezi, Italia wakitupwa nje michuano ya Euro 2024 kwa kichapo cha mabao 2-0 na Uswisi.**



"Ningependa kuendelea kucheza milele, lakini pengine itakuja wakati ambapo ni lazima nitunze buti zangu. Nitaendelea kucheza, lakini sijui kwa muda gani," **nahodha wa Croatia, Luka Modric, mwenye umri wa miaka 38 kwa sasa.**



# TETESI 10 ZA USAJILI WACHEZAJI WANDANI


MANULA

Na Adam Fungamwango

KATIKA kipindi hiki cha usajili, akili za mashabiki wengi zipo kwa wachezaji wapya kutoka nje ya nchi.

**Mashabiki wengi hasa wa Tanzania, hupenda zaidi usajili wa wachezaji wapya wa kigeni kutoka nje ya nchi, hawaangalii sana wachezaji wandani ambao nao wamekuwa wakitoka klabu mojakwenda nyingine, labda wale ambao wameshakuwa maarufu.**

Pamoja na yote, wachezaji wa Kitanzania wamekuwa na mchango mkubwa kuifanya Ligi Kuu Tanzania Bara kuvutia.

Ndiyo maana hata kipindi hiki cha usajili baadhi yao wamekuwa wakitakiwa na klabu zingine, baada ya kuonyesha viwango vizuri ndani ya timu zao.

Katika makala haya tunakuletea tetesi 10 za usajili wa wachezaji wa Kitanzania ambao wanatakiwa na klabu mbalimbali za Ligi Kuu na kwa asilimia kubwa huenda wakajiunga nazo, twende sasa...

**1. Aishi Manula - Azam**

Hizi bado ni tetesi mpya kabisa ambazo zimetoka juzi, zikieleza kuwa golikipa mahiri wa Klabu ya Simba, Aishi Manula, huenda akavaa jezi za Azam FC msimu ujao.

Habari zinasema kuwa Simba imeingia makubaliano na Azam kumtoa kwa mkopo katika kile linachoonekana kusafisha wachezaji waliokaa kwa muda mrefu na kutengeneza kikosi chenye wachezaji wengi wapya. Awali ilisemekana angekwenda Singida Big Stars, lakini mambo yamegeuka.

**2. Khomein Aboubakar - Yanga**

Tetesi zinasema Yanga wamekamilisha usajili wa golikipa wa Singida Black Stars, Khomein Aboubakar na kilichobaki ni kutangazwa tu.

Kipa huyo anakwenda kusaidiana na Djigui Diarra kwa kile kinachoelezwa kuwa Metacha Mnata anaondoka kwenda katika klabu hiyo ambayo mwenzake anatoka.

**3. Omari Omari - Simba**

Inaelezwa kuwa Simba wamekamilisha usajili wa mchezaji, Omari Omari kutoka Klabu ya Mashujaa FC.

Tetesi zinasema kinachosubiriwa ni kutangazwa tu, lakini mchezaji huyo wa zamani wa Prisons kabla hajahamia Mashujaa, anayecheza kama winga, kiungo mshambuliaji na wakati mwingine straika,ameshamalizana na Wekundu wa Msimbazi hao.

**4. Denis Mkane - Mashujaa FC**

Kuelekea Ligi Kuu ya msimu ujao Klabu ya Mashujaa imeelezwa iko katika hatua za mwisho za kumtwaa winga wa Yanga, Denis Nkane kwa mkopo.

Nkane ambaye amebakisha mwaka mmoja na mabingwa wa Tanzania Bara, anatakiwa na Mashujaa kwa kile kilichoelezwa kuwa anaweza kuwasaidia kwani amekuwa hapati namba kwenye kikosi alichopo, wakiamini bado ana uwezo mkubwa.

**5. John Bocco - JKT Tanzania**

Endapo mambo yataenda kama yalivyopangwa, Klabu ya JKT Tanzania itamtangaza straika mkongwe nchini, John Bocco kuwa mchezaji na nahodha wa timu hiyo.

Habari zilizopatikana juzi kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema, licha ya kwamba nahodha huyo wa Simba mpaka mwishoni mwa msimu uliomalizika amepewa kazi ya kukinoa kikosi cha vijana chini ya miaka 17, lakini mabosi wa JKT Tanzania wamekuwa wakimshawishi arejee uwanjani wakiamini bado ana uwezo mkubwa.

**6. Ayoub Lyanga - Singida Big Stars**

Winga huyu aliyepewa mkono wa kwaheri na Azam FC hivi karibuni, bado ameonekana lulu kwa baadhi ya klabu nchini, ambapo Singida Big Stars inatajwa inahitaji saini yake kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chao msimu ujao.

**7. Tepsie Evance - Azam FC**

Azam inadaiwa ipo mbioni kumrejesha mchezaji wake, Tepsie Evance, ambaye msimu uliopita alichezea KMC kwa mkopo.

Baadhi ya viongozi wa timu hiyo wanahitaji kumbakisha kijana huyo anayecheza winga na beki wa pembeni aliyekulia kwenye akademi ya klabu hiyo, licha ya kuwa na shutuma za utovu wa nidhamu, ambapo dili hilo linasubiri baraka za kocha Youssouph Dabo, kuamua.

**8. Awesu Awesu - Yanga**

Tetesi zinasema Yanga inataka kumchukua kiungo mshambuliaji, Awesu Awesu, kutoka KMC ili kuimarisha eneo la kiungo mshambuliaji.

Habari zinasema usajili huu ni pendekezo la kocha Miguel Gamondi ambaye ameonekana kuvutiwa na kiwango cha mchezaji huyo, alipomuona katika mechi mbili za Ligi Kuu ambazo timu hizo zilikutana.

**9. Ibrahim Ajibu - JKT Tanzania**

Tetesi zilizotoka jana zinadai kiungo mshambuliaji wa Coastal Union, Ibrahim Ajibu, yupo kwenye mazungumzo na mabosi wa JKT Tanzania kwa ajili ya usajili msimu ujao.

Ajibu, kiungo wa zamani wa Simba, Yanga, Azam na Singida Fountain Gate, anatajwa kwenda huko kutokana na ukaribu wake na wachezaji aliowahi kucheza nao Simba, Said Ndemla na Shiza Kichuya.

**10. Reliants Lusajo - Dodoma Jiji**

Straika asiyetulia timu moja, Reliants Lusajo anatajwa kutakiwa na Dodoma Jiji ambapo mazungumzo yanakwenda vizuri.

Lusajo, akishirikiana na Adam Adam aliyetangazwa rasmi kuwa ni mchezaji wa Azam FC, na Omari Omari anayetajwa kusajiliwa Simba, ndiyo kwa kiasi kikubwa walioibeba Mashujaa FC baada ya kusajiliwa kipindi cha dirisha dogo na kuinusuru kushuka daraja.

**JE, WAJUA?**

UEFA EURO2024 GERMANY

KATI ya mataifa 24 kwenye michuano ya Euro 2024, ni nchi moja tu ya Serbia ambayo imefunga mabao machache kuliko England - moja ambayo walifanikiwa ni katika sare ya bao 1-1 dhidi ya Slovenia, huku Ujerumani ikifunga mabao nane, Austria sita, na Ureno, Uhispania, Uswizi na Uturuki zote kila moja ina mabao matano.



## Wajasiriamali wanawake wapewe elimu matumizi mtandao

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

WAJASIRIAMALI na wafanyabiashara wanawake nchini bado wanahitaji kusaidiwa elimu ya kutumia mitandao ya kijamii ili kuuza na kuagiza biashara zao ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Women in Management Africa (WIMA), Dk. Naike Moshi alisema hayo juzi jijini hapa wakati wa hafla ya kujadili na kusherehekea ujasiri na mafanikio ya wanawake katika sekta ya biashara za kati na ndogo nchini.

Dk. Moshi alisema kundi la wanawake wajasiriamali na wafanyabishara ndogo na kati wanahitaji kusaidiwa katika kutumia mitandao ya kijamii katika kuagiza na kuuza biashara zao.

"Tunatakiwa kusaidiana katika kutumia mitandao hii ya kijamii kuuza biashara zetu pamoja na kuagiza mizigo ya biashara ndani na nje ya nchi" alisema.

Alibainisha kuwa mitandao hiyo ikitumika vizuri itasaidia kuongeza uchumi wa wanawake wengi hapa nchini.

Pia, alisema wanawake wakiagiza mizigo kwa kutumia mitandao itasaidia kutumia muda mwingine kuhudumia familia zao.

Kadhalika, alisema WIMA wapo kwenye safari ya kuongeza uelewa na uwezo wa watunga sera kuhusu matatizo yanayoikabili biashara ndogo na kati zinazoongozwa na wanawake wajasiriamali.

Alieleza kuwa pia shirika hilo linalenga kujadili mikakati ya kuchochea ukuaji wao wa biashara.

Dk. Mosi aliongeza kuwa lengo lao ni kuchangia kwa kiasi kikubwa kuwatambua wanawake wajasiriamali kama wadau muhimu kwenye kukuza uchumi wa nchi.

Aidha, alisema lengo lingine la WIMA ni kutoa msaada wa elimu na uwezo kwa ajili ya wajasiriamali wanawake na kuwasaidia kukua na kustawi kiuchumi.

Kadhalika alisema kuwa wanalenga kuimarisha uwezo wa kundi hilo katika kutoa mipango na rasilimali za kuongeza uwezo wa wajasiriamali na viongozi wao.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Mkoa wa Dodoma, Maryrobini Mabhaya ambaye alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule alilishukuru shirika hilo kwa kusaidia kundi la wanawake.

# Idadi matukio ya ukatili nchini yaongezeka 2023

**Na Thobias Mwanakatwe,**
MKALAMA

IDADI ya matukio ya ukatili nchini imeongezeka kutoka 18,403 mwaka 2022 hadi kufikia 22,147 yaliyoripotiwa mwaka jana.

Kamishna wa Kamisheni ya Polisi Jamii, CP Faustine Shilogile, alisema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa jengo la dawati la jinsia na watoto yaliyojengwa katika wilaya za Ikungi na Mkalama kwa ushirikiano wa UN Women na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Korea (KOICA).

Alisema katika matukio ya watoto mwaka 2023 yaliripotiwa 15,301 kulinganisha na matukio 12,162 yaliyoripotiwa mwaka 2022.

Shilogile alisema moja ya sababu ya kuongezeka kwa vitendo hivyo ni kutokana na uelewa mkubwa wa jamii katika kuripoti matukio ya ukatili kulinganisha na miaka ya nyuma.

Mkuu wa Wilaya ya Mkalama, Moses Machali alisema ujenzi wa majengo hayo ni juhudi ya serikali kwa kushirikiana na wadau katika kutokomeza ukatili wa kijinsia nchini.

Hivyo, aliwataka wakazi wilayani Mkalama kuhakikisha wanakuwa mstari wa mbele katika mapambano dhidi ya ukatili wa kijinsia.

"Kila mmoja ahakikishe anapambana kutoa taarifa kuhusu ukatili wa kijinsia kwenye mamlaka zinazohusika, tutumie Jeshi la Polisi vizuri. Sisi sote tunapaswa kuwa mashujaa katika mapambano haya", alisema.

Aidha, aliwasisitiza wazazi kuwapeleka watoto wao shule ili waweze kutimiza ndoto zao za kimaisha na mzazi atakayekataa serikali itamchukulia hatua kali.

Naibu Mwakilishi Mkazi, UN Wowen, Katherine Gifford alipongeza Jeshi la Polisi nchini na serikali kwa kuwa mstari wa mbele katika kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini.




Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Women in Management Africa (WIMA), Dk. Naike Moshi akizungumza wakati wa kongamano la kusherehekea mafanikio ya wanawake katika sekta ya biashara za kati na ndogo nchini, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanachama NHIF, ZHSF mambo safi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar (ZHSF), zimesaini mkataba wa makubaliano wa utoaji huduma za matibabu kwa wanachama wao.

Mkataba huo unalenga kutoa huduma kwa wanachama wa ZHSF kupitia vituo vilivyosajiliwa na NHIF Tanzania Bara kuanzia leo.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa maamuzi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuhakikisha wananchi wake wanapata huduma za matibabu wanapozihitaji bila kikwazo.

Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga alisema hatua hiyo ni katika kuhakikisha ZHSF inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar Na. 1/2023.

"Na kwa kutambua uzoefu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), katika uendeshaji wa mfumo wa bima ya afya nchini, Julai Mosi, 2024 ZHSF itaanza rasmi majukumu yake kwa kuhudumia wanachama na wategemezi wake kupitia vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa na NHIF Tanzania Bara"alisema Konga.

Alisema ili kufanikisha huduma kwa wanachama hao, NHIF na ZHSF zimesaini mkataba wa makubaliano wa mashirikiano katika utoaji wa huduma kwa wanachama wake.

"Hatua hii inatokana na uzoefu, wigo mpana wa vituo vya kutolea huduma vilivyosajiliwa na NHIF nchi nzima"alisisitiza Konga.

Alisema NHIF, imekamilisha hatua mbalimbali za maandalizi na utayari wa kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa mashirikiano ili kuhakikisha wanachama hao wanapata huduma bila ya changamoto yoyote.

Alisema hatua ilizokamilisha NHIF ni pamoja na kutoa taarifa kwa watoa huduma wote kuhusu suala hilo na kuwa tayari kuwahudumia wanachama.

Alisema pia ofisi zote za NHIF zilizoko mikoani ziko tayari na zimejipanga kutoa huduma na kutoa msaada utakapohitajika.

"Mifumo ya utambuzi imeimarishwa zaidi ili kurahisisha utambuzi wa wanachama wanapofika katika vituo vya kutolea huduma, kufanya malipo kwa watoa huduma kwa wakati pindi wanachama hawa watakapopata huduma za matibabu katika vituo husika, kuandaa ofisi kwa aiili watumishi wa ZHSF watakaokuwa wanahudumia wanachama kwa upande wa Tanzania Bara" alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa ZHSF, Yaasin Juma, alisema kwa mujibu wa Kifungu cha 27 cha Sheria Na 1 ya 2023, Mfuko umepewa uwezo wa kuwafikishia wanachama wake huduma za afya nje ya Zanzibar.

Alisema kwa kuanzia ZHSF imeanza kuwafikia wanachama wake walioko Tanzania Bara.

"Tukio la leo linaakisi utekelezaji wa masharti ya sheria hiyo. Hivyo basi, mafanikio haya ya kufikia makubaliano na wenzetu wa NHIF ni ya kujivunia kwani yatawawezesha wanachama wetu kupata huduma za afya wakiwa Tanzania Bara kwa kutumia kadi za ZHSF" alisema.

Alisema wanategemea mashirika yao kama ZIC, PBZ ambayo yanafanya kazi Tanzania Bara na wategemezi ambao wachangiaji wao wapo Zanzibar watafaidika na huduma hizo.





# Wakulima kufundishwa mbinu za kilimo kwa vitendo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TIJA ya uzalishaji wa mazao mbalimbali nchini inatarajiwa kuongezeka kutokana na kuanzishwa kwa mtaala mpya wa kuwafundisha wakulima kwa vitendo mbinu bora za kilimo, hivyo kuwaondoa kwenye kilimo cha mazoea.

Mtaala huo unaandaliwa kwa ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) cha mkoani Morogoro kwa kushirikiana na shirika la Care International ambalo ndilo linawezesha uandaaji wa mtaala huo kwa kuwafundisha wahadhiri.

Mkuu wa Kitengo cha Kilimo na Maendeleo ya Jamii cha Chuo cha SUA, Dk. Innocent Mathias aliyasema hayo kwenye maonyesho ya mashamba darasa ya kilimo biashara ambayo yameandaliwa na Chuo cha Kilimo cha Malti Uyole.

Alisema shirika hilo linaandaa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo wahadhiri wa chuo hicho kuhusu uandaaji wa mashamba darasa, ili wawafundishe wakulima kwenye maeneo yao kulingana na aina ya mazao wanayotaka.

Alisema wahadhiri hao wanafundishwa mbinu za kisasa za kilimo ili wakawasaidie wakulima hasa kulima kilimo biashara na pia waweze kuzalisha kwa tija na kuwa na uhakika wa chakula na ziada waiuze.

"Kwahiyo tunaandaa mtaala ambao sasa tutawafundishia wanafunzi wetu na pia tutautumia kwenda kuwafundisha wakulima katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuwasaidia kuzalisha kwa tija na kuongeza uchangiaji wa pato la taifa," alisema Dk. Innocent.

Mkurugenzi Mkazi wa Care International Tanzania, Prudence Masako alisema Tanzania imekuwa nchi ya kwanza kati ya nchi 34 ambazo shirika hilo linafanya kazi kuzipokea mbinu za shirika hilo na kuanza kuzifanyia kazi.

Alisema katika mataifa mengine mbinu hizo zinafanyiwa kazi lakini Tanzania imekuwa ya kwanza kutokana na chuo kikuu chake kimojawapo kuchukua teknolojia hizo na kuanza kuziingiza kwenye mtaala wa kufundishia.

Alisema moja kati ya sababu zilizosababisha Tanzania kuwa nchi ya kwanza ni ushirikiano ambao shirika hilo limeupata kutoka kwa viongozi mbalimbali wa serikali pamoja na SUA.

Vilevile, alisema sababu nyingine ni hali ya amani na utulivu iliyopo kwa maelezo kuwa watu wanafanya kazi za uzalishaji bila kuwa na misigano kama ilivyo kwenye mataifa mengine yenye mgogoro.

"Kwahiyo sisi kama shirika tunajivunia Tanzania kuwa nchi ya kwanza kupokea mbinu hizi za shamba darasa kwa vitendo, nchi zingine zote 34 ambazo tunafanya nao kazi zimepokea lakini kwa Tanzania ni tofauti kwa sababu mpaka chuo kikuu kimezipokea teknolojia zetu," alisema Prudence.

Baadhi ya wakulima na wakuu wa taasisi za kilimo walioshiriki maonyesho hayo waliahidi kwenda kuzitumia mbinu walizojifunza kuzalisha mazao mbalimbali kwenye maeneo yao na kuendelea kutembelea mashamba darasa kwa vitendo ili kujifunza.

Mkuu wa Chuo cha Kilimo cha Igurusi ilichopo wilayani Mbarali katika Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Lwesha alisema chuo hicho kiliwapeleka wanafunzi wake kwenye maonyesho hayo ili wajifunze kwa vitendo.

Alisema ushiriki huo utawarahisishia wakati wa kuwafundisha kwa maelezo kuwa mbinu nyingi watakuwa tayari wanazijua na hivyo kazi haitakuwa ngumu.

Alisema watazitumia pia mbinu walizojifunza kwenda kuwafundisha wakulima wa maeneo ya jirani na chuo hicho ili na wao waongeze tija kwenye uzalishaji.



Mwendesha pikipiki akipakia madumu ya maji kwa ajili ya kwenda kuyauza ili kujipatia riziki, katika Kijiji cha Mjele, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# 450 wenye matatizo ya macho wafanyiwa upasuaji

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WANANCHI zaidi ya 450 wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya waliokuwa wanakabiliwa na matatizo ya macho wamepatiwa matibabu ikiwemo kufanyiwa upasuaji wa mtoto wa jicho pamoja na kupatiwa miwani.

Walipatiwa matibabu hayo kwenye kambi maalumu ya wiki moja ya madaktari bingwa wa macho iliyoandaliwa wilayani humo, kwa ufadhili wa shirika lisilokuwa la kiserikali la Hellen Keller International.

Meneja wa mradi huo wa matibabu kwa wananchi kutoka Hellen Keller, Athuman Tawakal alisema madaktari walioshiriki kwenye kambi hiyo ni kutoka katika hospitali mbalimbali za Mkoa wa Mbeya.

Alisema wengine walikuwa wanatoka katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya ambao ndiyo walikuwa wanaongoza kambi, kutoka katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya pamoja na kutoka katika Hospitali za Wilaya za Chunya na Songwe.

Alisema walifanikiwa kufanya kambi hiyo kutokana na ushirikiano ambao walipata kutoka katika Wizara ya Afya na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

"Watu wanaobainika kuwa na mtoto wa jicho wanafanyiwa upasuaji na wanaobainika kuwa na matatizo yanayopaswa kupewa miwani wanapatiwa, lakini pia inasaidia kubaini ukubwa wa tatizo la macho katika mkoa huu," alisema Tawakal.

Hivyo, aliishukuru serikali kwa kuruhusu kambi hiyo kufanyika kwenye majengo ya hospitali ya serikali pamoja na kuruhusu madaktari bingwa kwenda kushiriki kwenye utoaji wa matibabu.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Dk. Elizabeth Nyema aliushukuru uongozi wa shirika hilo kwa kuendesha kambi hiyo akieleza kuwa inasaidia kurejesha furaha kwa wananchi wenye matatizo hayo ya macho.

Alisema kuna baadhi ya watu ambao walikuwa hawajawahi kuona lakini kwa sasa wanaona baada ya kufanyiwa matibabu na kwamba baadhi walikuwa na uoni hafifu lakini nao wameshapona.

## Madiwani Njombe wakerwa upigaji katika halmashauri

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

BARAZA la Madiwani la Halmashauri ya Mji Njombe, limetoa onyo kali kwa baadhi ya watumishi wa halmashauri hiyo ambao wamekuwa wakifuja fedha za umma.

Limesema litawachukulia hatua kali ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani na kurejesha fedha hizo.

Hayo yamebainika katika kikao cha baraza maalumu la madiwani wa Halmashauri ya Mji Njombe lililolenga kujadili hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka 2022/23.

Akisoma hoja ambazo hazijafungwa mwekahazina wa Halmashauri ya Mji Njombe, Edward Msangi alisema kuna hoja ya mwaka 2018/2019 ambapo aliyekuwa mtumishi wa halmashauri hiyo kudaiwa kutumia fedha za ushuru zaidi ya Sh. milioni 20 baada ya kuzikusanya.

Naye Ofisa Utumishi wa Halmashauri hiyo, Twilumba Mwalongo alisema mtumishi huyo ameshindwa kulipa deni lote kwa muda mrefu na amefukuzwa kazi kutokana na kukosa ndugu wa kumlipia.

Akifafanua taarifa ya mtumishi huyo, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Njombe, Kuruthum Sadiki aliwaomba madiwani kuridhia kufukuzwa kazi kwa mtumishi huyo na kusamehewa deni ili hoja ifungwe, kwani hata ikiendelea kuwepo itakaa muda mrefu na hakuna wakumlipia deni mtumishi huyo.

Awali Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari aliitaka ofisi ya mkurugenzi kushirikiana na baraza la madiwani kuyafanyia kazi mapungufu yanayosababisha kutokea kwa hoja haswa kwenye ukusanyaji wa mapato.



## Uhamiaji watakiwa kuzingatia mipango ya serikali

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi, Hamza Hassan Juma, ameitaka Jeshi la Uhamiaji kufanya kazi kwa kuzingatia programu zinazoendana na mipango ya serikali.

Alitoa agizo hilo wakati akifungua kikao cha maofisa wa Jeshi la Uhamiaji Zanzibar, kueleza kuwa serikali huanzisha miradi tofauti ikiwemo utanuzi wa viwanja vya ndege na bandari za kisasa ambazo utendaji wake unategemea taratibu za uingiaji na utokaji wa watu.

Alisema kutokana na hali hiyo kuna umuhimu kwa maofisa wa jeshi hilo kuhakikisha majukumu yao yanazingatia programu za serikali katika utaribu wa uingiaji na utoaji wa watu hapa nchini.

Hamza alisema utaratibu wa kufanya vikao hivyo utasaidia kujitathmini, utasaidia kuimarisha utendaji kazi hivyo wazingatie zaidi mahitaji ya wakati ikiwemo kuongeza ubunifu katika kukusanya mapato na kulipa umuhimu suala la ujenzi wa makazi ya askari hao ili kuleta ufanisi.

Pia, alilipongeza jeshi hilo kwa kuwa na mkakati wa kujenga nyumba za makazi kwa ajili wa wafanyakazi wao ambako kutasaidia kuongeza ufanisi.

Aidha, alilitaka Jjeshi hilo kuhakikisha inatoa fursa za masoma kwa vijana ili kuendana na mabadiliko yanayotokea.

Naye, Kamishna wa Uhamiaji Zanzibar, Hassan Ali Hassan, alisema malengo ya mkutano huo ni kujadiliana na kutafuta namna bora ya kuimarisha utendaji na utekelezaji malengo ya jeshi hilo, ikiwemo uendelezaji wa miradi ya majengo ya ofisi zao katika wilaya mbali mbali.

Alisema kwa mwaka 2024/2025 wameweka malengo kadhaa ikiwemo kuwa na nyumba za makazi pamoja majengo ya ofisi za uhamiaji kwa Unguja na Pemba.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni kusogeza huduma kwa wananchi ambapo kipindi kirefu huduma hizo hazikuwa karibu na wananchi.

Aidha alisema wanatarajia kujenga Chuo cha Uhamiaji, ambapo kwa mipango iliyopo chuo hicho kitajengwa eneo la Kitogani Wilaya ya Kusini ambapo matayarisho ya ujenzi huo yamefikiwa asilimai 80.

Akizungumza kwa niaba ya watendaji wenzake, Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhamiaji, Muhsin Abdallah Muhsin, aliaomba maofisa wenziwe kuongeza juhudi ili kupata matokeo bora, ikiwemo kudhibiti uhamiaji haramu na kuongeza mapato yatakayosaidia kuleta maendeleo ya nchi.

# Makamu wa Rais akemea majungu, uchawa kazini

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema miongoni mwa tabia mbaya kwenye utumishi wa umma zinazorejesha nyuma maendeleo ya nchi na kukatisha tamaa wafanyakazi ni baadhi ya watendaji na viongozi kujihusisha na majungu na uchawa.

Pia, amesema viongozi na watendaji serikalini wanawajibu wa kuviendeleza na kuvilea vipaji vya wafanyakazi wanaowasimamia.

Aliyasema hayo wakati wa hafla maalum ya kumuaga aliyekuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Dk. Omar Dadi Shajak, aliyestaafu baada ya kutumikia kwa miaka 33 ya nafasi ya ukatibu mkuu katika wizara mbali mbali.

Othman alisema viongozi na watendaji wana wajibu wa msingi wa kuwafunza na kuwapa miongozo wafanyakazi walio chini yao, ili kusaidia kupatikana watendaji wazuri watakaosaidia nchi kupata mafanikio ya kimaendeleo.

Alisema ni vigumu Zanzibar kupiga hatua kimaendeleo bila ya kuwepo watendaji wazuri wenye sifa na uwezo wa kuitumika vyema majukumu yao kwa uadilifu na uaminifu mkubwa.

Alisema kwamba Zanzibar ina watu wengi wenye vipaji na sifa kubwa, ambao wanapaswa kuendelezwa kiujuzi ili wafikie viwango vya juu vya weledi na kutumia maarifa yao kwa ajili ya kuisaidia nchi ifikie malengo ya kuwaletea wananchi maendeleo.

Othman alisema viongozi wanapaswa kuacha uchoyo katika kuwasaidia wafanyakazi waliochini yao, kuwapa maarifa ili wafikie viwango vya weledi, lakini wanapaswa kuhakikisha wasimamia maslahi hayo.

Aliwakumbusha wafanyakazi kutambua kuwa dunia ya sasa ni ya ushindaji kiutendaji, hivyo kinachohitajika ni kutayarishwa kiuweledi na ujuzi utakaosaidia kuongezeka kwa ufanisi na wanapostaafu waache alama njema.

Hivyo, aliwataka wafanyakazi na viongozi kujiongeza na kuiga mfano wa watendaji wema walioacha alama na sifa njema kwa kuitumika nchi kwa uadilifu mkubwa kama alivyofanya Dk. Shajak ambaye amesifiwa na viongozi wakuu wa nchi kwa uadilifu na uaminifu aliokuwa nao wakati wote akiitumikia nchi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harous Said Suleiman, aliwakumbusha viongozi waliopewa dhamana katika utumishi wa umma kuwa na tabia ya ubinadamu kwa wafanyakazi wanaowaongoza.

Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Zena Ahmed Said, alisema siyo jambo jema kwa watumishi wanaostafu ama wanaoondolewa kazini waliobaki kushereheka kwa kupikiwa pilau kutokana na mambo mabaya walioyafanya kwa watumishi wengine badala ya wafanyakazi kusikitikia.




Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT), Prof. Elifas Bisanda (kushoto), akizungumza wakati wa uzinduzi wa kamati ya ushauri ya viwanda ya chuo hicho, chuoni hapo, Dar es Salaam jana. Katikati ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo hicho (Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Kitaalamu), Prof. Alex Makulilo na Mkurugenzi wa Elimu ya Juu kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Peter Msofe. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# ZECO, PBZ zakubaliana uuzaji umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SHIRIKA la Umeme Zanzibar (ZECO), limeingia mkataba na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), unaolenga kutanua wigo wa uuzaji wa nishati ya umeme visiwani hapa.

Hafla hiyo ilifanyika ofisini ya ZECO Gulioni, ambapo Meneja Mkuu wa shirika hilo, Haji Mohammed Haji, alisema hatua hiyo itasaidia kufanikisha kutoa huduma bora na kuondoa usumbufu kwa wananchi.

Alisema kuwa hapo awali umeme ulikuwa unauzwa baina ya kampuni ya simu ya Tigo/Zantel na ZECCO, ambapo hivi sasa serikali imeamua kuwa huduma za uuzaji umeme zitanuliwe kwa kila mdau ambae atapenda kutoa huduma hiyo.

Alisema hatua hiyo itasaidia kupunguza gharama za uendeshaji kwa shirika hilo za kuuza umeme kwa sababu mpaka sasa ina vituo vinane kwa Unguja na Pemba, ambavyo vinauza umeme moja kwa moja kwa wananchi.

Meneja huyo alisema mfumo huo ulikuwa unawapa gharama kubwa ZECO kwa kulazimika kila ifikapo jioni kukusanya mapato na kuzipeleka katika vituo vikuu kabla ya kupelekwa benki.

"Suala hili lilikuwa linachangia gharama kubwa za uendeshaji lakini vile vile kuna hatari hutokea katika ukusanyaji wa hizo fedha sambamba na kuwalipa walinzi wanaosimamia kukusanya fedha hizo kwa ajili ya kuzileta katika kituo chetu kikuu", alisema.

Alisema kuwa ili kukabiliana na suala hilo wameamua kuongeza wigo wa uuzaji ambapo kampuni walizokubaliana nao watauza kwa wananchi wa kawaida kwa kutumia wakala wao.

"Kwa sasa si lazima uwe na simu kununua umeme, unaweza kwenda kwa wakala wa benki wa kampuni za mawasiliano na ukanunua umeme moja kwa moja," aliongeza.

Alisema kwa hatua hiyo watavifunga vituo vya uuzaji umeme kuanzia Julai mwaka huu na kubakisha vituo vilivyopo makao makuu Gulioni na Chake Chake Pemba.

Hata hivyo, alisema ifikapo Julai mwaka huu ZECO itapunguza gharama za uuzaji unuaji umeme.

Naye Mkurugenzi wa Biashara kutoka PBZ, Eddie Mhina, alisema lengo la kuingia mkataba huo ni kusogeza huduma kwa wananchi ili kuleta maendeleo.


Alisema watumiaji wa PBZ wanaweza kununua umeme kupitia huduma ya benki ya simu pamoja na mawakala wao ambao uuzaji wa umeme utakuwa kwa gharama nafuu.

Mkurugenzi wa kampuni ya Tigo-Zanztel, Arnold Ngalashi, alisema makubaliano hayo yanaashiria hatua kubwa ya ufikiaji wa umeme kwa wananchi, mashirika na taasisi ambapo serikali itachukua hatua ya kurahisisha shughuli za kijamii na kiuchumi.

Kampuni ambazo zinatarajiwa kuingia mkataba huo ni pamoja na Tigo /Zantel, CRDB, NBC, NMB na TTCL.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAPHAEL AUGUSTINE LYARUU** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **NP 0345/0125/2019** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **USAGALA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2019. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA : **PHQ/DAR/UBU/117182/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RAHMA R KISUO** anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo kozi ya **BACHELOR OF LAWS** chenye namba ya usajili **TU/DARCO/LLB/016/237** kilichotolewa na **DAR ES SALAAM TUMAINI UNIVERSITY** mwaka 2019,yeyote atakaye kiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **PHQ/DAR/ILA/16290/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GASPER B.MFOY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S1880-0177** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **MBEZI HIGH** mwaka 2017,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **PHQ/DAR/UBU/129051/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA MWANGA**

**UTHIBITISHO NA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**SHAURI LA MIRATHI NA 13628 YA MWAKA 2024**
**MAOMBI YA BARUA YA USIMAMIAJI WA MIRATHI YA**

**GEOFREY LUIWANA MREMA..................MAREHEMU**

**YUNISI FATAELI MOSHA..........................MUOMBAJI**

**TAARIFA KWA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki katika mirathi ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa barua ya usimamiaji wa mirathi kwa muombaji aliyeomba hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikwa mnamo au kabla ya tarehe 20 Mwezi Agosti, Mwaka 2024.

Imewasilishwa Mwanga leo tarehe 20 Mwezi JUNI Mwaka 2024.

DISTRICT COURT MWANGA

HAKIMU MKAZI MKUU
MAHAKAMA YA WILAYA
MWANGA
Hakimu Mkuu Mkazi Mfawidhi
Mwanga

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI NA BAJAJI

**ABRAHMAN ALLY NASSORO** anatangaza kupotea kwa kadi za pikipiki aina ya **SANLG** na **BAJAJI** aina ya **BOXER MC 895 BBG, T 221 CJJ, MC 121 BJS, MC 512 BPL, MC 222 BQH, MC 765 BQS, MC 251 BTD, MC 711 BVC, MC 785 CHF, MC 129 CXR.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**PHQ/DAR/ILA/127976/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya mwanzo ya wilaya ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na. 24 /2024**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA**
**MAREHEMU ATHUMANI ALI KINGWELE WA CHAMWINO MJINI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI**
**YALIYOLETWA**
**NA SHABANI ATHUMANI ALI KINGWELE**

**TANGAZO**
**( Kanuni ya 5(@) ya kanuni za usimamizi wa mirathi mahakama za mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/ maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 18 mwezi 07 mwaka 2024 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa marehemu anaweza kuuleta mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 6 mwaka 2024

**Summons to appear (O.V, R.20(1) OF (Civil procedure code)**
**(substituted service)**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**

**AT DAR ES SALAAM**

**LAND CASE NO. 26059 OF 2024**

**PENUEL HILDER LAISER....................................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & OTHERS ..................DEFENDANTS**

**TO:**
1. FIS AFRICAN STARCH DEVELOPMENT COMPANY LIMITED
2. ALLAN NALIGIA MAGOMA
3. IBRAHIM MICHAEL HAPE
4. MAZIKU BUNDARA
5. DEONATUS JULIUS MALEGESI
6. MARWA MTALA
7. EDWIN PANCRAS KATO
8. RONALD SYLVESTER RWEGASIRA

**WHEREAS:** The above named plaintiff has instituted the SUIT against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on 18th day JULY, 2024 at 12:00 PM for HEARING of 1st PTC Before Hon, S. MWAIPOPO, judge to answer the said SUIT nad you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to reply insupport of your reply.
**TAKE NOTICE** that , in default of your appearance on that day, the said matter will be heard and determined in your absence.
Given under my hand and the seal of this court , this 20th day of JUNE, 2024

DEPUTY REGISTRAR

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MASJALA NDOGO YA TEMEKE**

**(TEMEKE KITUO JUMUISHI HUDUMA ZA MAHAKAMA MIRATHI NA NDOA)**

**MIRATHI NA 14471 YA MWAKA 2024**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU ROSEMARY MABEL KIGADYE**
**NA**
**RICHARD KIGELI KIGADYE ......................MWOMBAJI**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**( kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia shauri hili katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua ya usimamizi wa mirathi kwa mwombaji hapo juu.
Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 12 mwezi Saba, 2024. Saa 02:00 asubuhi . siku ambayo shauri hili limepangwa kusikilizwa mbele ya **Mhe. Jaji M. MNYUKWA.**
Imesainiwa Dar es salaam, leo tarehe 21 Mwezi wa Juni, 2024.

NAIBU MSAJILI

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO. 14941 OF 2024**

**In the Matter of the Estate of the Late:**
**PETER ANTHONY KWEMBE**

**By 1: BERNADA PETER KWEMBE**
**2: ______________________**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 18TH day of JULY.2024

Dated at MOROGORO this 27TH day of JUNE.2024

MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO

RESIDENT MAGISTRATE
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
DISTRICT COURT
P.O.Box 660,Morogoro

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE DISTRICT DELEGATED COURT OF MOROGORO AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE No. OF 2024**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE;-**
**STELLA MKENDA MAGANGA..............DECEASED**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR A LETTER OF ADMINISTRATIX BY;-**
**SAMWEL LEFI MAGANGA..........PETITIONER**

**GENERAL CITATION**
**(Made under rule 75 of the probate and Administration of Estate rules, CAP 352 R.E 2019)**

ALL person claiming to have any interest in the estate of the above-named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 04th day of July.2024.
Dated at Morogoro this .27th day of .June 2024.

Dated at Morogoro this .27th day of .June 2024
Senior Resident Magistrate
Morogoro District Court
MOROGORO
SENIOR RESIDENT MAGISTRATE DISTRICT COURT P.O.Box 660,Morogoro

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO, MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# M23 waiteka Kanyabayonga

**KINSHASA,** DRC

WAASI wa M23 wameuteka mji wa kimkakati wa Kanyabayonga katika eneo linalokabiliwa na machafuko la mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Ofisa tawala, aliyezungumza kwa sharti la kutokutajwa jina, alisema jana kuwa mji wa Kanyabayonga umekuwa mikononi mwa waasi wa M23 tangu Ijumaa jioni.

Mji huo unapatikana Kaskazini mwa Kivu na kwamba umekuwa ukikabiliwa na machafuko tangu 2021 wakati M23 walipoanza tena kampeni yao ya mashambulizi ya silaha katika eneo hilo. Mji huo pia unachukuliwa kuwa njia muhimu kuelekea vituo vikubwa vya kibiashara mjini Butembo na Beni upande wa kaskazini.

Pia eneo hilo linatajwa kuwa na wakazi zaidi ya 60,000 pamoja na maelfu ya watu waliolazimika kuyakimbia makazi yao katika miezi ya hivi karibuni, wakifukuzwa kutoka kwenye nyumba zao na waasi wanaosonga mbele.

"Watu wako huko hasa wale ambao walihamia kutoka eneo la Rutshuru hadi Lubero. Hawana tena mahali pa kwenda, ni ukiwa kamili, umma umechoka," alisema ofisa huyo.

Mkazi mmoja aliliambia shirika la habari la Ufaransa, AFP, kwamba waasi wa M23 waliwaomba wakazi waendelee kukaa Kanyabayonga wakati wa mkutano uliofanyika katikati ya mji uliofanywa na msemaji wa kundi hilo, Willy Ngoma.

"Watafika Kinshasa, tutaendelea kukimbia hadi umbali gani?" aliuliza mkazi huyo, akiongeza kwamba waasi wanaahidi amani.

Mtawala wa kijeshi wa eneo la Lubero, Kanali Alain Kiwewa, alisema wanaona ongezeko la watu wasio na makazi kutoka Miriki, Kirumba na Luofu kuelekea kaskazini, na kwamba hali hiyo inawatia wasiwasi.

**MAPIGANO YAONGEZEKA**

Duru za kuaminika katika eneo hilo zilisema mapigano kati ya vikosi vya Kongo na waasi yalikuwa yanaongezeka katika maeneo yanayouzunguka mji wa Kanyabayonga. Na kwamba watu walio nje ya mji huo pia walishuhudia mapigano hayo.

Kiongozi wa vijana katika mji wa Kayna, alisema usiku kucha risasi zilirindima, na kwamba wale ambao walikuwa wamekuja mjini humo kutokea Kanyabayonga walilala nje usiku kucha na walijawa na hofu.

"Hatufahamu tena ni mtakatifu yupi wa kumgeukia," alisema.

Kiongozi mwingine wa shirika la kijamii, alisema mji wa Kirumba ulioko kilometa 25 kutoka Kanyabayonga, umma uko katika hali ya taharuki.

"Hatuwezi kusogea kwenda kokote, tutakwenda wapi? Hatujui kwa kwenda," alisema.

Ofisa wa Umoja wa Mataifa (UN) anaeshughulikia masuala ya haki za binadamu, katika ripoti yake ya kila mwezi iliyotolewa juzi, alisema kuwa makabiliano yanasababisha wananchi kuyakimbia makazi yao. **DW**

# 30 wadaiwa kuuawa Kenya

**NAIROBI,** Kenya

SHIRIKA la kutetea haki za binadamu la 'Human Rights Watch' limesema karibia watu 30 walifariki katika maandamano ya wiki iliyopita yaliyochochewa na mapendekezo ya serikali kuhusu kuongeza ushuru wa bidhaa.

Katika taarifa ya Human Rights Watch iliyotolewa juzi, ilisema maofisa wa usalama waliwafyatulia risasi waandamanaji Juni 25 mwaka huu wakiwemo waliokuwa wakiwatoroka polisi.

Licha ya kwamba hakuna idadi rasmi ya watu waliouawa katika miji iliyoshuhudia maandamano, Human Rights Watch ilibaini kwamba idadi hiyo ya watu waliuawa siku hiyo kwa mujibu wa taarifa kutoka kwa umma, takwimu za hospitali na makarani jijini Nairobi.




Otsieno Namwaya, Ofisa wa Human Rights Watch barani Afrika alitoa wito kwa mamlaka nchini Kenya kuwaeleza maofisa wake wa polisi kwamba wanastahili kuwa wanawalinda wananchi wanaoandamana kwa amani na kwamba vitendo vya uhuni wa polisi havikubaliki.

Maandamano hayo ambayo kwa sehemu kubwa yalikuwa yakifanyika kwa amani siku ya Jumanne ya wiki iliyopita, yaligeuka kuwa vurugu muda mfupi tu baada ya wabunge kupiga kura kuidhinisha muswada wa kuongeza ushuru wa bidhaa mbalimbali.

Baada ya wabunge kuupitisha muswada huo, waandamanaji walivamia bunge ambako walichoma moto sehemu ya majengo ya bunge.

Utawala wa Rais William Ruto ulilazimika kuondoa muswada huo kutokana na shinikizo kutoka kwa waandamanaji waliokuwa wakiupinga.

Kwa upande mwingine, shirika la kutetea haki za binadamu linalofadhiliwa na serikali ya Kenya lilisema lilikuwa limerekodi vifo 22 na majeruhi 300 likisema kwamba litaanzisha uchunguzi. **RFI**



Maofisa wanaosimamia uchaguzi nchini Iran wakiendelea na maandalizi ya uchaguzi huo. **PICHA: MTANDAO**

# Wairan kufanya uchaguzi Julai 5

**TEHRAN,** Iran

WANANCHI nchini Iran watafanya duru ya pili ya uchaguzi wa rais ili kuamua ni nani atachukua nafasi ya kiongozi wa zamani hayati Ebrahim Raisi.

Ofisa mmoja wa tume ya uchaguzi nchini humo alibainisha hayo juzi baada ya duru ya kwanza ya zoezi hilo, lililofanyika mwishoni mwa juma lililopita, kutobaini mshindi wa moja kwa moja.

Uchaguzi wa Ijumaa wiki ijayo utawajumuisha mgombea mpenda mageuzi Masoud Pezeshkian dhidi ya mwenye msimamo mkali aliyekuwa mtetezi wa mpango wa nyuklia wa Iran, Saeed Jalili.

Mohsen Eslami, msemaji wa tume ya uchaguzi alitoa matokeo hayo katika mkutano na waandishi wa habari uliorushwa na televisheni ya taifa ya Iran.

Alisema kati ya kura milioni 24.5 zilizopigwa, Pezeshkian alipata milioni 10.4 huku Jalili akipata milioni 9.4. Spika wa Bunge Mohammad Bagher Qalibaf milioni 3.3, na kiongozi wa dhehebu la Kishia Mostafa Pourmohammadi 206,000.

Ilielezwa kuwa sheria za Iran zinahitaji kwamba mshindi apate zaidi ya asilimia 50 ya kura zote zilizopigwa. Ikiwa sivyo, wagombeaji wawili bora wa kinyang'anyiro hicho, watafuzu kwa duru ya pili wiki moja baadaye.

Kumekuwa na uchaguzi mmoja tu wa marudio wa urais katika historia ya Iran, mwaka 2005, wakati Mahmoud Ahmadinejad mwenye msimamo mkali alimshinda Rais wa zamani Akbar Hashemi Rafsanjani.

Eslami alikiri Baraza la Walinzi la nchi hiyo litahitaji kutoa idhini rasmi, lakini matokeo ya awali hayakuleta changamoto yoyote ya haraka kutoka kwa wagombea katika kinyang'anyiro hicho.

Kama ambavyo imekuwa tangu Mapinduzi ya Kiislamu ya 1979, wanawake na wale wanaotaka mabadiliko makubwa wamezuiwa kugombea, na waangalizi wanaotambuliwa kimataifa hawaruhusiwi kuwepo. **VOA**

# ZANZIBAR YATAKA KUWA KITOVU CHA MICHEZO AFRIKA MASHARIKI

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imedhamiria kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya michezo kwa kushirikiana na sekta ya utalii hapa nchini lengo likiwa ni kuona inakuwa kitovu cha michezo Afrika Mashariki.

**Hayo yalielezwa juzi, Jumamosi na Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Mudrik Ramadhan Soraga, katika hafla ya utoaji tuzo kwa waliofanya vizuri msimu huu wa Ligi Kuu Zanzibar, iliyoandaliwa na Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), na kufanyika visiwani hapa.**

Alisema kumekuwa na juhudi mbalimbali zinazofanywa na serikali ambazo matarajio yao ni kuona kunakuwa na maendeleo katika sekta hiyo muhimu ambayo imekusanya vijana wengi.

Soranga alisema Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anajitahidi kufanya mapinduzi hayo kwa kuimarisha miundombinu ya michezo ikiwamo ujenzi wa viwanja.

"Inatoa faraja kubwa kuona tuna mwelekeo mzuri katika michezo, hasa kwa kuwa sekta ya michezo na utalii ni sawa na watoto pacha, dhamira yetu ni Zanzibar kuwa kitovu cha michezo kwa Afrika Mashariki," alisema.

Alisema hayo yote yatafanikiwa iwapo kutakuwa na ushirikiano baina ya sekta hizo mbili pamoja na wadau wengine wa michezo.

Aidha, alipongeza wadhamini wa ligi hiyo Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ ) na Azam Media ambao bila ya michango yao wasingefika hapo walipo.

Mapema Kamishna wa Idara ya Michezo Zanzibar, Ameir Mohammed Makame, aliwaomba wadau kudhamini na michezo mengine ikiwamo ya watu wenye ulamavu, wanawake ili nao washiriki vema mashindano yao.

Alisema serikali imekuwa ikijitahidi kujenga miundombinu mbalimbali ya michezo ili kuona watu wake wanashiriki michezo kila wilaya na mikoa kwa maana ya mjini na vijijini.

Naye Meneja Masoko wa PBZ, Self Suleiman, alisema wataendelea kuongeza nguvu kila mwaka na kuleta maendeleo katika sekta ya michezo.

Alisema tangu kuwa wadhamini wamepata maendeleo makubwa na bado wana Safari ambayo wanaitarajia kuijenga ili ligi zijazo ziwe bora zaidi.

"Kila mwaka tutakuwa tunaangalia wapi penye mapungufu ili kuboresha, lakini tunajivunia mpaka mafanikio ambayo tumeyapata hadi sasa," alisema Seif.

Rais wa ZFF, Dk. Suleiman Mahmoud Jabir, alisema wanajukumu la kuhakikisha soka la Zanzibar linaendelea vizuri na kuwa bora kwa kila msimu.

Alisema jitihada zake ni pamoja na kuhakikisha wanapata wadhamini zaidi, kwani waliopo wamewasaidia pakubwa na uwapo wao umekuwa chachu na ndio sababu ya kuonekana yale ambayo yanafanyika.

Tunzo mbalimbali zilitolewa katika usiku huo ikiwamo tuzo za heshima, muhamasishaji, shabiki, mwandishi, msemaji, mwamuzi kijana, mwamuzi bora, kamisaa, mwamuzi wa pembeni, goli bora, mchezaji bora kijana na timu yenye nidhamu.

Tunzo nyingine ni kipa bora, beki bora, kiungo bora, mshambuliaji bora, kocha bora, kikosi bora, mchezaji bora wa ligi ambaye ni Suleiman Mwalimu Abdalla wa KVZ pamoja na vyeti maalum kwa watendaji wa ZFF na tuzo wa wadhamini.




Mshambuliaji wa Peru, Edison Flores, akimiliki mpira dhidi ya beki wa kushoto wa Argentina, Nicolas Alejandro Tagliafico, kwenye mechi ya Copa America iliyopigwa Marekani jana. Argentina ilishinda 2-1. **PICHA: MTANDAO**

## Choki bingwa Dar Boxing Derby

**Na Shufaa Lyimo**

BONDIA Juma Choki ameibuka bingwa wa pambano la Dar Boxing Derby 2024 (Tagi la Mama Samia), baada ya kumchakaza vikali mpinzani wake, Nassib Ramadhani, katika mpambano huo uliofanyika jana, kwenye viwanja vya Posta Kijitonyama, Dar es Salaam.

Choki aliibuka mshindi kwenye baada ya kumchakaza mpinzani wake, Ramadhani kwa pointi katika pambano hilo lillilokuwa la raundi nane. Akizungumza baada ya ushindi huo, Choki alisema amefurahi kuibuka bingwa kwani haikuwa kazi rahisi kutokana na upinzani ulioupata.

"Mchezo ulikuwa mgumu isipokuwa ninashukuru nimeweza kumpiga mpinzani wangu na kuwa Bingwa wa Dar Boxing Derby 2024," alisema Choki.

Aidha, alimpongeza mwandaaji wa pambano hilo, Meja Selemani Semunyu, kwa kueleza kwamba amekuwa akiwasaidia vijana wengi kupata riziki pamoja na kuonyesha vipaji vyao kupitia mapambano mbalimbali anayoyaandaa.

Kwa upande wa Nassibu Ramadhani, alisema amefanya makosa ambayo yamemlazimu kupokea kichapo hicho na kuahidi kwenda kujipanga upya.

Pambano hilo lilishirikisha mabondia wa kike pamoja na wa kiume ambapo lengo lilikuwa ni kupata bingwa wa 'Derby' hiyo.

Kwa upande wa wanawake Nasra Msami naye alishinda kwa pointi baada ya kumpiga mpinzani wake, Nasma Isike kwenye pambano hilo lillilokuwa la raundi sita.

Baada ya kumalizika kwa pambano hilo Nasra alisema amefurahi kupata ushindi huo na kuweka wazi licha ya kushinda bado anamkubali mpinzani wake huyo.

Naye mwandaaji wa pambano hilo, Meja Semunyu, aliwapongeza mabondia wote walioshiriki katika pamoja na kuwashukuru mashabiki kwa muitikio mkubwa waliouonyesha, kwa kujaza viwanja hivyo.

# Klabu za Ligi Kuu Bara zamgombea Ntibazonkiza

**Na Adam Fungamwango**

LICHA ya Klabu ya Coastal Union kuanza kuonyesha nia ya kuitaka saini ya kiungo mshambuliaji raia wa Burundi, Saido Ntibazonkiza, jumla ya klabu nne zimejitokeza kupigana nao vikumbo zikihitaji huduma yake.

Habari za ndani kutoka Coastal Union zinasema tayari kumeshazuka ugumu kwani klabu nne zimeshaingiza mguu zikiisaka saini yake, hivyo thamani yake kupanda sokoni.

Klabu zinazotajwa kujitosa kumwania ni Namungo FC na Dodoma Jiji, pamoja na mbili zilizopanda Ligi Kuu, Pamba na KenGold.

"Tunaendelea na mazungumzo naye, lakini kuna timu nazo zimeingia zinamhitaji, sasa ikishakuwa hivyo hata yale mazungumzo ya mwanzo yanabadilika kabisa, mlikubaliana hivi mnakuta kuna kitu kingine kabisa na mkisema mkatae, basi wenzenu ndiyo wanachukua.

"Ila kwetu sisi Saido ana umuhimu zaidi kuliko hao wengine, sisi tunakwenda kucheza Kombe la Shirikisho Afrika, hizi zingine zitacheza Ligi Kuu tu, kwa hiyo sisi ndiyo tunaopaswa kukaza msuli ili tumchukue," alisema mtoa taarifa huyo ndani ya klabu hiyo.

Coastal kwenye dirisha hili la usajili imekuwa ikipambana kusaka saini za wachezaji wa kigeni wazoefu kwa kile ilichoeleza wanataka kufanya vema katika Kombe la Shirikisho Afrika ambalo itacheza msimu ujao.

Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Abbas El Sabri, amesema usajili wanaoufanya kuelekea msimu ujao ni wa wachezaji wa wazoefu na wa kimataifa tu na si vinginevyo.

"Mchezaji tunayemsajili ni lazima awe amecheza Ligi ya Mabingwa au Kombe la Shirikisho ili watusaidie kwenye michuano ya kimataifa inayotukabili. kuna wachezaji wengi wa kimataifa wazuri tu ambao tunazungumza nao, hivi ninavyokwambia kuna beki wa Timu ya Taifa ya Uganda yupo nchini kwa ajili ya kukamilisha usajili, siwezi kutaja jina lake kwa sasa kwani hiki ni kipindi cha usajili na kuna timu kazi yao ni kuchukua tu wachezaji wanaoletwa na klabu zingine," alisema.

Baadhi ya wachezaji wanaotajwa kuwa huenda wakatua Tanga ni Mukoko Tonombe kutoka TP Mazembe ambaye yupo nchini kwa sasa, Djuma Shaaban na Tuisila Kisinda ambao wote wameshawahi kuichezea Yanga.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DE LIGT ATAKIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imeanza mazungumzo na beki wa kati wa Uholanzi, Matthijs de Ligt, 24, ambaye yuko tayari kuondoka Bayern Munich msimu huu wa majira joto. ***(Sky Sport Germany)***

### YAMAL AWANIWA PSG

PARIS St-Germain iko tayari kulipa ada ya uhamisho iliyovunja rekodi ya dunia kumsajili winga wa Hispania, Lamine Yamal mwenye umri wa miaka 16, kutoka Barcelona. ***(Mundo Deportivo)***

### KIMMICH ATAJWA MAN CITY

KLABU ya Manchester City ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Bayern Munich na Ujerumani, Joshua Kimmich, 29, na winga wa RB Leipzig kutoka Hispania, Dani Olmo, 26. ***(Sun)***

### JACKSON KUJUMUISHWA

CHELSEA imejadili kumjumuisha mshambuliaji wa Senegal, Nicolas Jackson, 23, kama sehemu ya mkataba wa mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak, 24. ***(Sun)***

### HAG SAFI MAN UTD

MAZUNGUMZO kati ya Klabu ya Manchester United na kocha, Erik ten Hag, kuhusu mkataba mpya yamekuwa mazuri na yamepiga hatua wiki hii. ***(Sky Sports)***

### LUKAKU PAUNI MILIONI 37

CHELSEA inataka pauni milioni 37 kwa ajili ya mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku, 31, lakini AC Milan na Napoli wanatumaini kwamba bei ya mchezaji huyo itashuka msimu huu wa majira ya joto. ***(Gianluca di Marzio)***

### ALVAREZ LULU BARCA, PSG

BARCELONA na Paris St-Germain zinatumaini kumshawishi mshambuliaji wa Argentina, Julian Alvarez, 24, kuondoka Manchester City msimu huu. ***(Caught Offside)***

### LOOKMAM SASA ANYATIWA

JUVENTUS inanamnyatia mshambuliaji wa Atalanta, Ademola Lookman, 26, huku Bayern Munich wakimfanya mchezaji huyo wa Nigeria kuwaniwa na klabu kadhaa za Ligi Kuu ya England. ***(Mail)***

### TAH ANUKIA BAYERN

KLABU ya BAYERN Munich ipo kwenye mazungumzo ya kumsajili beki wa Ujerumani, Jonathan Tah, 28, kutoka Bayer Leverkusen na klabu hizo mbili zinakaribia kufikia makubaliano ya mchezaji huyo ambaye amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake. ***(Sky Sports Ujerumani)***

### ISAAK KUJIFUNGA TENA

NEWCASTLE United ina imani kwamba mshambuliaji wa Sweden, Alexander Isak, 24, atasaini mkataba mpya msimu huu wa majira ya joto, huku Chelsea wakionesha nia ya kutaka kumsajili. ***(Givemesport)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SPALLETTI AKUBALI LAWAMA ITALIA KUTOLEWA EURO 2024

**COLOGNE,** Ujerumani

KOCHA wa Italia, Luciano Spalletti, amesema alichukua jukumu kamili kwa timu yake kutolewa kwenye michuano ya Ulaya katika raundi ya kwanza ya mtoano baada ya kupoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Uswisi.

**Hata hivyo, bosi huyo wa zamani wa Napoli mwenye umri wa miaka 65, pia alilalamika kuwa hakuwa na mechi za kutosha za kuiunganisha timu yake kabla ya kichapo hicho, ambacho kiliashiria kuondolewa kwa Italia kwa mara ya kwanza kabla ya hatua ya robo fainali ya Euro katika kipindi cha miaka 20.**

"Nina jukumu," alisema Spalletti katika mkutano na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Tulishindwa kwa sababu ya uteuzi wa timu yangu."

> ●●● Tulishindwa kwa sababu ya uteuzi wa timu yangu, nilikuwa na siku 10 tu za kuiandaa...

Spalletti alisema, hakuwa na muda wa kutosha wa kuifahamu timu hiyo vema.

"Makocha wengine wote walikuwa na mechi 30 au hata zaidi na timu zao kabla ya mashindano kuanza," alisema, na kuongeza: "Nilikuwa na 10 tu."

Aliongeza: "Kuna uwezekano wa kujenga kitu, lakini inachukua muda kidogo zaidi. Sikuwa na mengi. Tukiangalia watangulizi wangu, karibu wote walikuwa na michezo mingi kuliko mimi."

Spalletti aliteuliwa kuwa kocha wa Timu ya Taifa ya Italia Agosti 2023, baada ya kujiuzulu kwa Roberto Mancini.

Alifanya mabadiliko sita kwenye safu yake ya mwanzo dhidi ya Uswisi, lakini badala ya kuingiza nguvu na ubunifu kwenye timu, walionekana kutoungana na bila uvumbuzi, na hawakuweza kupiga shuti kwenye lango.

Italia ililazimika kucheza bila mmoja wa wachezaji wao wa kuvutia sana nchini Ujerumani, beki aliyesimamishwa Riccardo Calafiori.

Mabao katika kila kipindi kutoka kwa Remo Freuler na Ruben Vargas yaliwapa Waswisi ushindi wao wa kwanza dhidi ya jirani yao kwa miaka 31 na kutinga robo.

"Bao la mwanzoni mwa kipindi cha pili lilikata miguu yetu, hatukuwa wachangamfu sana," Spalletti aliwaambia wanahabari.

"Kilicholeta tofauti ni kasi, tulikuwa na kasi ambayo ilikuwa duni sana kuliko wao kipindi cha kwanza, hata kwa mchezaji mmoja mmoja kulikuwa na kasi tofauti."

## HABARI MICHEZO



# VINICIUS ALALAMIKIA VIWANJA COPA AMERICA

**LAS VEGAS,** Marekani

VINICIUS Junior alikosoa viwanja vya Copa America, waamuzi na waandaji CONMEBOL baada ya kufanya vema katika mchezo wa ushindi wa mabao 4-1 wa Brazil dhidi ya Paraguay Ijumaa.

Mshambuliaji huyo wa Real Madrid alifunga mara mbili katika ushindi mnono kwenye Uwanja wa Allegiant, Las Vegas, na kuiacha Brazil ikiwa na pointi nne katika nafasi ya pili ya Kundi D - nyuma ya viongozi Colombia - na kufuzu kwa robo fainali.

"Copa America daima ni ngumu kwa sababu ya viwanja, kwa sababu ya waamuzi - ambao daima wanatupinga - na kwa sababu ya jinsi CONMEBOL inavyowatendea watu," alisema Vinicius baada ya mechi.

"Siku zote ni vigumu, lakini tunapaswa kuwa imara. Tunaweza kuzungumza kwa kushinda tu. Tunapozungumza, CONMEBOL wanasema tunazungumza sana."

Brazil ilitoka suluhu na Costa Rica Jumatatu, huku Vinicius akipewa shutuma kuhusu jukumu lake katika timu.

Hata hivyo, kocha Dorival Junior alimsifu fowadi huyo baada ya mchezo wake dhidi ya Paraguay.

"Nimecheza mchezo mzuri, kulingana na kiwango cha mchezaji nilicho nacho," alisema Vinicius.

"Vinicius ana namna ya kucheza ambayo si rahisi kwa wapinzani kukubali," alisema kocha huyo.

Hali ya viwanja kwenye Copa America - huku nyasi asili zikiwekwa juu ya nyasi bandia kwenye viwanja sita - imekuwa ikijadiliwa mara kwa mara kwenye mashindano hayo hadi sasa.



# Torres kubaki Barcelona

**BARCELONA,** Hispania

FERRAN Torres amesisitiza nia yake ya kusalia Barcelona baada ya msimu huu wa majira ya joto.

Ingawa hajapata nyakati nzuri zaidi akiwa na 'La Blaugrana' hao tangu alipowasili kutoka Manchester City mwaka 2022, Ferran bado ni mchezaji anayethaminiwa sana na klabu nyngi.

Hapo awali Arsenal walitajwa kuhitaji huduma yake, lakini lengo la hivi majuzi lilihusu Newcastle United, huku baadhi ya ripoti zikifikia kudai kwamba ofa ilikuwa imetolewa.

Akizungumzia ni wapi atakuwa kwa msimu wa 2024/25, Ferran aliiambia RAC1 kwa ujasiri: "Nitaendelea kuwania Barca.

"Nimetulia sana. Wanaweza kuhifadhi wino na kubadilisha jina langu kwa mtu mwingine, ni kwamba nitaendelea Barca."

Ferran alijiunga na Barca kwa mkataba wa miaka mitano hadi 2027, miamba hao wa Katalunya wakiweka kifungu chake cha ununuzi kuwa euro bilioni moja.

Inabakia kuonekana kama kocha Hansi Flick anaweza kupata matokeo bora kutoka kwa Ferran huku mchezaji huyo akihangaika chini ya bosi wa awali Xavi.

Alishiriki katika mechi 29 za La Liga msimu uliopita, lakini 12 pekee kati ya hizo alianza, ingawa Ferran bado alifanikiwa kurejesha kwa heshima mabao saba na asisti tatu, huku pia akifunga mara tatu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

# Kocha Denmark alia na VAR kwa Ujerumani

**DORTMUND,** Ujerumani

KOCHA wa Denmark, Kasper Hjulmand, alilalamikia "sheria za kipuuzi za kuunawa mpira" na kusema "hivi sio jinsi soka linavyopaswa kuwa" baada ya maamuzi mawili ya VAR ndani ya dakika mbili dhidi ya timu yake kusaidia wenyeji wa Euro 2024, Ujerumani kushinda 2-0 juzi.

Mwamuzi wa Ligi Kuu England, Michael Oliver, alikataa bao la Joachim Andersen dakika ya 48 baada ya kuingilia kati kwa VAR iliyoangazia kosa la kuotea la pembeni lililohusisha kiungo wa Denmark, Thomas Delaney.

Dakika mbili baadaye, Oliver alitoa penalti kwa Ujerumani baada ya maofisa wa VAR, Stuart Attwell na David Coote kumtaka ahakiki mpira wa mkono uliioguswa na Andersen kutokana na krosi ya David Raum. Kai Havertz alifunga mkwaju wa penalti na kuiweka Ujerumani mbele kwa bao 1-0, na Jamal Musiala kisha akaongeza la pili kwa wenyeji baadaye kipindi hicho.

Lakini Hjulmand mwenye hasira alihoji matumizi ya VAR baada ya mchezo na akabainisha kuwa maamuzi yote mawili yalikwenda kinyume kwa timu yake.

"Iliamuliwa na maamuzi mawili ya VAR," alisema Hjulmand.

"Nina picha hapa ya Delaney eti ameotea. Ilikuwa sentimeta moja. Haileti maana, hivi sivyo tunapaswa kutumia VAR.

"Na kisha baada ya dakika chache, ni penalti kwa Ujerumani. Nimechoshwa na sheria za kipuuzi za mpira wa mikono. Hatupaswi kuhitaji beki kucheza kwa mikono namna hii. Yeye Andersen alikuwa anakimbia kawaida, ni jambo la kawaida hali hiyo na alipigwa na mpira kutoka umbali wa mita moja.



## HABARI MICHEZO

## Meena, Masele waitwa Twiga Stars

**Na Somoe Ng'itu**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Bakari Shime, amewaita kwa mara ya kwanza katika kikosi hicho, Victoria Masele anayecheza TopHat Soccer Academy ya Georgia na Malaika Meena wa Forest University ya Marekani, imeelezwa.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema jana wachezaji hao wameitwa kwa ajili ya mechi za kirafiki za kimataifa dhidi ya Tunisia na Botswana zitakazofanyika hivi karibuni.

Ndimbo alisema wachezaji hao watawasili nchini hivi karibuni ili kuungana na nyota wengine wa timu hiyo watakaoingia kambini leo jijini Dar es Salaam.

"Kocha Shime amewaita wachezaji hawa ili kuongeza nguvu katika kikosi chake kwa sababu huko mbele tunahitaji kupata matokeo chanya kwenye mashindano yote ya kimataifa tutakayoshiriki," Ndimbo alisema.

Aliwataja wachezaji wengine walioitwa kuwa ni pamoja na Najat Abasi kutoka JKT, Asha Mrisho ( Amani), Lidya Maximilian (JKT), Protasia Mbunda (Fountain Gate), Enekia Kasonga (Eastern Flames), Julietha Singano (Mexico),

Vailet Mwamakamba ( Simba Queens), Anastazia Katunzi, Joyce Lema, Janeth Christopher (JKT), Ester Maseke (Bunda) na Diana Lucas wa Ame SKF.

Wachezaji wengine ni Aisha Juma (Simba Queens), Stumai Athumani, Winifrida Gerald (JKT), Maimuna Kaimu (ZED ya Misri), Elizabeth Charles ( Alliance), Aisha Masaka (BK- Hacken), Oppa Clement (Besiktas) na Clara Luvanga anayecheza Saudi Arabia katika Klabu ya Al Nasr.

Twiga Stars imefuzu kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake (WAFCON), ambayo yamesogezwa mbele na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), hadi Julai mwakani.

# AZAM KUMRUDISHA MANULA, YATANGAZA KIFAA KINGINE

**Somoe Ng'itu na Adam Fungamwango**

WAKATI ikimtangaza rasmi kiungo mshambuliaji, Nassor Saadun kutoka Geita Gold, Klabu ya Azam imetajwa kuwa katika harakati ya kumrudisha golikipa wa Simba, Aishi Manula, atakayekwenda kwa mkopo.

Habari zilizopatikana kutoka ndani ya klabu hizo mbili zinasema kumekuwa na mazungumzo ya pande mbili kuhusu kipa huyo ambaye aliwahi kuichezea Azam FC na kujiunga na Simba 2017.

Taarifa zinaeleza kuwa Azam inamhitaji Manula kutokana na uzoefu wake kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, huku viongozi wa Simba wakitaka kumuondoa ili kumsogeza Ali Salim kuwa kipa namba mbili na baadaye kumpa mikoba ya kuwa namba moja.

"Tuna kipa mzuri, Mohamed Mustapha, lakini Manula atatufaa zaidi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa, amecheza kwa kiwango kikubwa na kuifikisha Simba robo fainali mara tano, uzoefu wake ndiyo tunaouhitaji kwa sababu sisi lengo letu namba moja angalau kwanza tutinge hatua ya makundi, tumeona atatufaa na kwetu ni rahisi kumpata, pia ni mtoto wa nyumbani," alisema mtoa taarifa kutoka Azam FC.

Taarifa kutoka ndani ya Klabu ya Simba zinasema mabosi wa timu hiyo wanaona sasa ni wakati wa kuanza maisha mapya bila ya Manula ambaye mkataba wake unamalizika 2025, hivyo kumtoa kwa mkopo.

Habari zinasema awali ilikuwa apelekwe Singida Black Stars, lakini Azam imeonyesha nia ya kutaka kumchukua, hivyo mazungumzo yanaendelea ambapo huenda Simba nayo ikanufaika na dili hilo kwa kupata mchezaji.

"Salim ni kipa mzuri na mdogo, anatunzwa ili awe kipa namba moja wa Simba, na hata Taifa Stars, moja kati ya mipango ya kumfanya afikie huko ni kumuondoa Manula ambaye kwa sasa amepoteza imani kwa wanachama na mashabiki, bahati nzuri Ayoub Lakred ambaye amezolea sifa kwa mashabiki anabaki, Salim atakuwa kipa namba mbili, Hussein Abel yeye atakuwa kipa wa tatu," kilisema chanzo.

Wakati huo huo, uongozi wa Azam FC umemsajili kiungo, Nassor Saadun kutoka Geita Gold ya mkoani Geita.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', aliliambia gazeti hili jana Saadun amepewa mkataba wa mwaka mmoja na wenye kipengele cha kuongeza tena muda kama huo endapo wataridhishwa na kiwango chake.

Popat alisema wanaendelea kuboresha kila idara katika timu yao kwa sababu wanataka kufanya vema katika mashindano yote watakayoshiriki kwenye msimu mpya.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', akimshuhudia kiungo mshambuliaji wa Geita Gold, Nassor Saadun, akisaini mkataba wa kujiunga na klabu yao jana jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba yanyakua kocha Morocco

INATOKA UKURASA 24

ka Agosti 3, mwaka huu katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Awali Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed wakati akitangaza tarehe rasmi ya tamasha hilo, alisema watatangaza mbeleni timu itakayokuja kucheza na Simba siku ye kilele cha tamasha hilo Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Hata hivyo, taarifa kutiko ndani ya klabu hiyo zinaeleza kuwa Simba imetuma mwaliko kwa klabu hiyo ya Rwanda kuja Tanzania kucheza nao siku hiyo ya kuhitimisha Wiki ya Simba.

Taarifa kutoka Rwanda zimethibitisha klabu hiyo ya jeshi itakuja nchini kucheza na Simba baada ya kukubali mwaliko wa Wekundu hao.

Mtandao maarufu nchini humo (Inyarwanda.com) juzi uliandika, "Agosti 3, 2024, Simba SC watakuwa wenyeji wa APR FC katika mchezo maalum wa Simba Day."

Simba Day ni tamasha la kila mwaka ambalo Simba hulitumia kuwatambulisha wachezaji wake wapya na benchi zima la ufundi mbele ya mashabiki wao.

## Yanga yasubiri Aussems...

INATOKA UKURASA 24

ataamua," alisema Kanu.

Ingawa Kanu hakuweka wazi klabu gani zinawatataka wachezaji hao, taarifa za ndani zinasema, Tchakei na Kagoma wanatakiwa na Simba, Lobota amewavutia Yanga na Rupia huenda akatimkia Azam FC.

Kanu amebainisha kuwa kikosi hicho kitaanza rasmi kambi ya maandalizi ya msimu mpya Jumatano ambapo Aussems ataamua sehemu ambayo anataka timu ikajichimbie.

# Michezo

Jumatatu Julai 1, 2024

Nipashe





Torres kubaki Barcelona UKURASA 22

MATESO...




Kiungo mshambuliaji wa Ujerumani, Jamal Musiala, akiifungia timu yake bao la pili, huku kipa wa Denmark, Kasper Peter Schmeichel, akiteseka kuokoa bila mafanikio, kwenye mechi hiyo ya michuano ya Euro 2024 iliyopigwa Ujerumani juzi na wenyeji kushinda mabao 2-0. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YANYAKUA KOCHA MOROCCO

**Adam Fungamwango na**

**Faustine Feliciane**

## ●●● Kutambulishwa wiki hii huku rasmi sasa wakiikaribisha APR ya Rwanda...

KLABU ya Simba, wakati wowote inaweza kumtangaza raia wa Afrika Kusini, Fadlurraghman "Fadlu" Davids kuwa Kocha Mkuu wa kikosi hicho, atakayekinoa kwa msimu ujao wa mashindano, imefahamika.

**Taarifa za ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa, baada ya kikao cha juzi mabosi wa Simba kwa kauli moja wamekubaliana kumpa jukumu kocha huyo anayejulikana zaidi kwa jina la Fadlu Davids kuwa Kocha Mkuu ambaye atachukua jukumu la kuongoza kikosi hicho kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika, Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la FA.**

"Suala la Kocha Mkuu tumeshamaliza, tunamalizia baadhi ya watu wa benchi la ufundi na baadhi ya wachezaji wachache waliobaki," alisema mtoa taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo.

Fadlu anatua Simba akitoka kocha msaidizi wa kikosi cha Raja Casablanca ya Morocco, ambayo mpaka sasa ipo chini ya Josef Zinnbauer.

Kabla ya kuchukuliwa na klabu hiyo ya Afrika Kaskazini, kocha huyo alikuwa akiifundisha Maritzburg United ya Afrika Kusini, huku 2023 akiwa ni kocha msaidizi katika klabu Lokomotiv Moscow ya Urusi.

Klabu zingine ambazo amewahi kufundisha ni Orlando Pirates ya Afrika Kusini kama kocha mkuu 2021, ambapo kabla ya hapo alikuwa msaidizi kwenye klabu hiyo mwaka 2019, chini ya makocha watatu kwa nyakati toafauti, Zinnbauer ambaye baadaye walikutana Raja Casablanca, Milutin Sredojevic 'Micho', na kocha Rulani Mokwena, kocha wa sasa wa Mamelodi Sundowns.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Klabu ya Simba, Ahmed Ally, alisema suala la kocha linafanyiwa kazi na uongozi wa juu na likikamilika ataambiwa, na yeye atawahabarisha mashabiki.

Pamoja na hayo aliwatoa hofu wanachama na mashabiki wa Simba kuwa watakapoondoka nchini kwenda Misri, kwenye Jiji la Ismailia, watakuwa na benchi zima la ufundi.

"Safari hii niwaambie tu kuwa tutaondoka tukiwa kamili, kwa maana ya makocha wote, mkuu, msaidizi, wa makipa, wa viungo na meneja, kila mtu atakuwa kwenye nafasi yake, pia tutaondoka wote pamoja hapa hapa na wachezaji wote walioongezewa mikataba na wapya, kuelekea kambini kuanza 'pre season' yetu," alisema Ahmed.

Mbali na kocha huyo, Simba ilikuwa inahusishwa na makocha wengine ambao ni Florent Ibenge, ambaye juzi alisema kwa sasa hayupo kwenye mpango huo, Msauzi Steve Khompela na Mreno Alexandre Miguel Santos ambaye anaifundisha Petro de Luanda ya Angola.

Katika hatua nyingine imefahamika kuwa Simba itacheza mchezo wa kirafiki na APR ya Rwanda wakati wa Tamasha lao la Simba Day litakalofanyi-

INAENDELEA UKURASA 23

# Yanga yasubiri Aussems aamue

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu mpya wa Singida Black Stars, Patrick Aussems, anatarajia kuwasili nchini leo kwa kuanza rasmi kazi ya kukinoa kikosi cha timu hiyo kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano, huku akitarajia kuamua hatma ya wachezaji wa timu hiyo wanaotakiwa na Klabu za Simba na Yanga.

Kocha huyo ambaye amewahi kuifundisha Simba 2018 hadi 2019, alipewa kibarua cha kukiongoza kikosi cha timu hiyo kilichobadilisha jina kutoka Ihefu, baada ya kuachana na kocha wake, Mecky Maxime.

Mkurugenzi wa Ufundi wa klabu hiyo, ambayo zamani ikiitwa Ihefu, Muhibu Kanu, amesema, ujio wa kocha huyo mbali na kuanza rasmi kazi ya kufua kikosi hicho, lakini atatoa ripoti kama anaweza kuwaruhusu wachezaji wanaotakiwa na klabu mbalimbali, zikiwamo Simba na Yanga huku ofa zikiwa mezani.

Wachezaji wanaotakiwa kutoka kwenye klabu hiyo ni Elvis Rupia, straika kutoka nchini Kenya, kiungo mshambuliaji Marouf Tchakei raia wa Togo na Emmanuel Lobota, winga raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, na kiungo mkabaji, Yusuph Kagoma.

"Kuna ofa nyingi mezani, ipo ya Rupia kuna watu wametuma barua ya kuleta ofa, zipo mezani kwangu nimeziona kuna wanaomhitaji Tchakei kuna timu inamtaka Kagoma, hata Lobota, yaani klabu zinataka wachezaji wetu tofauti tofauti, ila tulichokuwa tunasubiri ni kwamba kocha aje, yeye ndiye atatoa ruhusa nani auzwe na nani abakishwe, au wote wabaki, au wauzwe wote wanaotakiwa ili tusajili wengine, kocha ndiye

INAENDELEA UKURASA 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >